# Nipashe

Jumamosi Agosti 15, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580311

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



## CCM kupuliza rasmi kipenga kampeni za urais Agosti 29

UKURASA 5




UKURASA 11

# Kanisa lataka uwazi kura uchaguzi mkuu

• **Kama** ilivyokuwa vyama vya siasa, lasema itaondoa malalamiko ya kushindwa, JPM ataka viogozi wa dini kuhamasisha waumini kupiga kura... *Endelea ukurasa 2*




Rais Dk. John Magufuli akionyesha tuzo ya heshima, baada ya kukabidhiwa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG), Dk. Barnabas Mtokambali (kushoto), alipohudhuria kilele cha mkutano mkuu wa kanisa hilo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### SARUJI YA TANZANIA YAPATA SOKO EAC, SADC

TANZANIA imepata neema ya soko kubwa la saruji kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile za Jumuiya...

UKURASA WA 5

### TCRA YASHUSHA RUNGU VYOMBO VYA HABARI

KAMATI ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imevishushia rungu vyombo vya habari vya...

## Sugu na wafuasi watiwa mbaroni

UKURASA 3




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

## CHADEMA yataka uchunguzi waliochoma ofisi za Arusha

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAIBUA MAZITO HUKUMU MORRISON UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abuobakar Kunenge, akimuapisha Ng'irabuzu Ludigija, kuwa Mkuu wa Wilaya ya Ilala, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TAG wataka uwazi uchaguzi mkuu 2020

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KANISA la Assemblies of God (TAG), limetaka kuwapo kwa uwazi katika uhesabuji kura na utangazaji wa matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kama ilivyofanyika kwenye mchakato wa kura za maoni ndani ya vyama vya siasa.

Katika Mkutano wa Baraza Kuu la Kanisa hilo uliohudhuriwa na Rais John Magufuli jijini Dodoma jana, Askofu Mkuu wa TAG, Dk. Barnabas Mtokambali, alisema wanaamini uchaguzi huo utaendeshwa kwa misingi ya haki na kuwapata viongozi bora.

"Wahenga walisema dalili ya mvua ni mawingu, tumeanza kuziona dalili nzuri za mvua za uchaguzi huru na wa haki hasa kupitia mchakato wa upatikanaji wa wagombea ndani ya vyama vya siasa ambao umeonekana kuwa wa wazi na wa kidemokrasia.

"Aliyeshinda anaonekana na aliyekosa anaonekana wazi wazi, hakuna nafasi ya hisia zozote za hila wala udanganyifu," alisema.

Askofu Mtokambali alimwomba Rais Magufuli kupitia serikali anayoongoza, kudumisha uwazi huo pia kwenye uchaguzi mkuu.

"Yaani kuhesabu kura na kutangaza matokeo kufuate utaratibu mzuri uliofanyika kwenye vyama ili kusitokee nafasi ya wale wepesi kudhani kuwa kila wanaposhindwa wanaibiwa kura," alishauri.

Alibainisha kuwa hatua hiyo itaweka mazingira ya amani na utengamano katika taifa.

"Tunamshukuru Mungu kwa kukuweka wewe kuwa Rais, baada ya kuleta kilio chetu serikalini tangu miaka ya sabini kuomba uchaguzi usifanyike siku ya ibada hatimaye kupitia kwako Mungu amejibu maombi," alipongeza.

Kiongozi huyo wa kanisa pia alimpongeza Rais kwa utendaji wake ambao umetikisa dunia na kuweka nidhamu serikalini na kwa wananchi.

"Sisi viongozi wa kiroho, tunaomba Mungu nchi ifike kwenye upevu wa kijamii, kiuchumi na kisiasa na Mungu akubariki kwa kazi hii uliyotutendea," alisema.

Hata hivyo, askofu huyo alisema kuna tatizo la mmomonyoko wa maadili hasa kwa vijana kutokana na kukosa uzalendo, kutoheshimiana, kuvaa mavazi yasiyo na heshima na kuthaminiana.

Aliwataka viongozi kuliona tatizo hilo na kuandaa mikakati ya kulitatua ili kulinusuru taifa kutumbukia kwenye baa la kuwa na wananchi waliokosa maadili mema.

# ...JPM: Viongozi wa dini wahamasishe kupiga kura

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli amewataka viongozi wa dini kuhamasisha waumini wao kushiriki katika uchaguzi mkuu, hasa siku ya kupiga kura Oktoba 28, mwaka huu.

Kiongozi huyo wa nchi alitoa rai hiyo alipohutubia mkutano mkuu wa Baraza Kuu la Kanisa la Asemblies of God (TAG) uliofanyika jijini hapa jana.

Alisema siku ya uchaguzi ni siku ya mapumziko na waendelee kumwomba Mungu wapatikane viongozi wenye maono.

"Wachapakazi na wazalendo kwa taifa letu, tusiangukie mikononi mwa viongozi wabadhirifu, wabinafsi au vibaraka maana kazi ya viongozi kama hao huwa ni kubomoa badala ya kujenga, kung'oa badala ya kupanda na kutawanya badala ya kukusanya," alisema.

Rais Magufuli alisema ni vyema wakamwomba Mungu awajalie hekima ya kufanya uamuzi sahihi.

"Katika baadhi ya nchi wakati mwingine zoezi la uchaguzi limekuwa chanzo cha kuzuka kwa vurugu na fujo. Kwa msingi huo, niwaombe viongozi wa dini kuliombea na kuliweka mikononi mwa Mungu taifa letu ili tumalize salama uchaguzi wetu huku tukiendelea kubaki na amani, umoja na mshikamano.

"Kwangu mimi ninaliona taifa la Tanzania ni muhimu zaidi kuliko mifarakano ya mambo mengine," alisisitiza.

Aliwahakikishia viongozi hao kuwa serikali imejipanga kuona uchaguzi mkuu unakuwa wa huru na wa haki.

Aliwasihi wanasiasa kufanya kampeni za kistaarabu na kutotumia lugha za kuwatisha wananchi.

"Niwaombe Watanzania tuwakatae wanasiasa wenye kuhubiri chuki na kutoa maneno ya vitisho, wanafanya hivyo kwa sababu hawana sera na wanajua vurugu zikitokea wao wanapo mahali pa kwenda kuishi," alisema.

"Dini isitugawe, vyama visitugawe, wala makabila yasitugawe, tuishi tukijua tuna Mungu ambaye ni mtawala wa dunia yote, tuna imani kuwa mkisimama tutavuka salama," alisema.

Rais Magufuli alieleza kufurahishwa na kusanyiko la maaskofu na wachungaji takribani 4,000 waliohudhuria mkutano huo uliodhihirisha uwapo wa Mungu na aliwashukuru viongozi hao kwa kazi kubwa wanayoifanya kuliombea taifa na kutoa huduma za kijamii kupitia shule na vyuo, vituo vya watoto yatima na watoto wa mitaani, miradi ya maendeleo na visima vya maji vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini.

Pamoja na kulipongeza kanisa hio, Rais Magufuli pia aliahidi kuwa serikali itaendelea kulinda uhuru wa kuabudu ambao upo kwa mujibu wa katiba na itaendelea kutoa ushirikiano katika juhudi mbalimbali za kanisa hilo kuhudumia jamii ikiwamo ujenzi wa chuo kikuu jijini Dodoma, akimwagiza Mkuu wa Mkoa Dk. Binilith Mahenge kuhakikisha mpango huo unafanikiwa na uwekezaji mwingine wowote ambao kanisa hilo litaona unafaa kuufanya.

"Ninafikiri msiishie tu kujenga chuo, ila mnaweza kutenga eneo lingine ili muanzishe ujenzi wa viwanda, ninawahakikishia kuwa serikali inatambua na kuthamini mchango wenu hivyo tunaahidi kuendelea kushirikiana nanyi kwa karibu sana," alisema.

Alisema serikali itaendelea kutengeneza mazingira mazuri ili taasisi za dini kuendelea kuchangia maendeleo ya nchi katika uwekezaji.

Rais Magufuli aligusia mafanikio mbalimbali yaliyopatikana ikiwamo kukarabati treni ya kwenda mkoani Arusha ambayo ilisimama kwa zaidi ya miaka 20.

"Miradi yote tunayoifanya nchini ni kwa mapenzi makubwa ya Mungu wetu ambaye tuna wajibu wa kumtumikia kupitia kuwatumikia wananchi na kuwatatulia changamoto zao,"alisema.

Katika hatua nyingine, Rais Magufuli alishukuru kwa tuzo maalum ya heshima kutoka kwa baraza hilo kwa kutambua jinsi alivyoliongoza taifa kumtegemea Mungu katika kipindi kigumu cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapatu inayosababishwa na virusi vya corona, maarufu Covid-19.

Katika mkutano huo, Askofu Mkuu na Mwenyekiti wa Baraza Kuu la TAG ambaye pia ni Rais wa Shirikisho la Makanisa ya Assemblies of God barani Afrika, Dk. Barnabas Mtokambali, alimkabidhi Rais Magufuli tuzo hiyo kutambua namna alivyoliongoza taifa kumtegemea Mungu katika kipindi hicho cha mlipuko wa virusi hivyo.

HABARI KITAIFA



Katibu wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Mkoa wa Dar es Salaam, Sheikh Swed Twaib (kushoto), akijadiliana jambo na baadhi ya viongozi wenzake, katika kikao cha kutangaza kongamano kubwa la kuombea amani kuelekea uchaguzi mkuu litakalofanyika jijini Dodoma Agosti 24, mwaka huu, kilichofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Kutoka kulia ni Mjumbe wa Taifa, Hamisi Mbaruku, Mwenyekiti Wilaya ya Ilala, Askofu Lilian Baitani na Kiongozi wa Kata ya Kivule, Shamsa Kyombo. **PICHA: MUHIDINI MSAMBA**

# CHADEMA wataka uchunguzi waliochoma ofisi zao Arusha

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimeitaka serikali kuwakamata wahalifu waliochoma ofisi ya chama hicho Kanda ya Kaskazini.

Kwa mujibu wa Jeshi la Polisi, ofisi hizo zilizoko jijini Arusha, zilichomwa moto usiku wa kuamkia jana na kusababisha uharibifu wa samani zilizokuwamo na miundombinu ya jengo la ofisi hizo.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Bara, Benson Kagaila, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa, tukio hilo lilitokea majira ya kati ya saa nane na saa tisa usiku.

Kigaila alidai majirani wa ofisi hiyo walisikia kelele za mlinzi wa ofisi hizo akiomba msaada na baadaye sauti hiyo ilipotea.

Alisema mlinzi wa ofisi hiyo ambaye alidaiwa kutekwa, amepatikana.

"Walioliona jengo, wanasema lilimwagiwa petroli na kuchomwa moto, tunajiuliza sababu ni nini na kwanini ifanyike hivyo," Kigaila alisema.

Aliongeza kuwa, iwapo serikali haitawapata ndani ya siku tano waliohusika na tukio hilo, CHADEMA itawatafuta na kushughulika nao.

"Wanalenga kutisha watu ili waogope kwenda kwenye mikutano, kwenda kudhamini mgombea urais, hatutatishwa, chama hakijafa na kina nguvu kuliko ilivyokuwa zamani, kwenye uchaguzi huu tunakwenda sawa," alidai.

KAULI YA POLISI

Kamanda wa Polisi Mkoa Arusha, Salum Hamduni, alithibitisha kuteketezwa kwa moto kwa ofisi hizo majira ya usiku wa kuamkia jana.

"Bado tunaendelea na uchunguzi wa tukio hilo, lakini tukio lenyewe lilitokea majira ya saa tisa usiku katika ofisi hizo zilizoko katika eneo la Kimandolu jijini.

"Niwaombe wananchi kutoa ushirikiano kwa jeshi hili, ili kubaini waliochoma moto ofisi za CHADEMA ili kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Vitu vilivyoteketea ni viti, mito ya makochi, ambayo yalikuwa kwenye baraza la nyumba hiyo na kuvunjwa vioo vya madirisha sita ya nyumba hiyo. Jambo hili tunalichunguza ili kubaini wahusika kwa ajili ya kuwafikisha katika vyombo vya sheria," alisema.

Kamanda Hamduni alisema kuwa hadi wakati huo, hapakuwa na mtu aliyekamtwa kuhusiana na tukio hilo, akiahidi kutoa taarifa kwa vyombo vya habari baada ya vyombo vya dola kukamilisha uchunguzi wake. Kuhusu madai ya kutekwa kwa mlinzi, Kamanda Hamduni alisema Jeshi la Polisi halikuwa na taarifa juu ya suala hilo.

Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Arusha, Reginald Masawe, alisema wamesikitishwa na tukio hilo, lakini hakuwa tayari kulizungumzia zaidi, akiacha jukumu hilo kwa uongozi wa chama kitaifa.

"Baada ya kufanya tathimini ya vitu vyote vilivyoteketea, viongozi wetu watazungumza kwenye ngazi hiyo, ila siyo mimi, imetusikitisha sana tukio hili ambalo limetokea wakati tunampokea Makamu Mwenyekiti wetu wa taifa, Tundu Lissu," alisema. Licha ya kutokea kwa kuchomwa kwa ofisi hizo, umati mkubwa wa watu ulijitokeza jana kwenye eneo hilo kumdhamini Lissu aliyechukua fomu kwenye Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuomba kuteuliwa kuwania nafasi ya urais katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

***Imeandikwa na Romana Mallya (DAR) na Daniel Sabuni (ARUSHA)**

# Sugu akamatwa akichukua fomu kugombea ubunge

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MGOMBEA ubunge katika Jimbo la Mbeya Mjini kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi, na wanachama 15 wamekamatwa na polisi kwa tuhuma za kufanya maandamano kinyume cha sheria.

Majira ya saa 6:00 mchana, wafuasi wa CHADEMA pamoja na Mbilinyi, maarufu kama Sugu, walifika katika ofisi ya chama zilizoko Kata ya Sinde kwa lengo la kuanza pamoja safari ya kumsindikia katika ofisi za Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kuchukua fomu kuwania nafasi hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alikiri Sugu na wenzake kukamatwa na kwamba lengo ni kupewa elimu juu ya mambo ya kuzingatia katika msimu huu wa kuelekea uchaguzi na kwamba wakati wa kufanya maandamano bado kwa sababu tume haijatoa majina na kibali cha kuanza kufanyika kwa kampeni, hivyo wangesubiri utaratibu. "Nilipata taarifa kuwa Sugu leo (jana) anakwenda kuchukua fomu kwa maandamano makubwa ambayo yalianzia mitaa ya Sinde na wanachama hao waliamua kumsindikiza hadi ofisi za tume licha ya kutopewa kibali lakini pia kulikuwa na vurugu ambazo wanachama walizifanya walipofika katika ofisi za NEC," alisema Matei.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kukabidhiana fomu na kabla Sugu hajatiwa nguvuni, Msimamizi wa Uchaguzi ambaye pia ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Ademe Ng'wanidako, alisema alitimiza wajibu wake wa kumkabidhi fomu ili kwenda kuijaza na kutafuta wadhamini.

"Mimi kazi yangu tayari nimeitekeleza kwa kutoa fomu kwa mgombea. Kinachofuata akatafute wadhamini na kuzirejesha. Kuhusu kukamatwa kwa wafuasi wa chama hicho hizo ni habari nyingine," alisema. Katibu wa CHADEMA Mkoa wa Mbeya, George Tito, alisema kwa sasa wanashughulikia suala la dhamana na kujua sababu za kukamatwa kwa Sugu na wanachama wengine na kusisitiza kuwa maandamano ni kitu cha kawaida kwa kuwa wananchi ni wapigakura wake.

Tito alisema CHADEMA inalaani vikali kitengo kiichofanywa na Jeshi la Polisi kwa kuwa ni kuminya uhuru wa kidemokrasia katika kuelekea uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, kwa kuminya vyama upinzani na kufanya udhalilishaji wa hali ya juu.

"Kama chama tunaendelea kutafakari tukio hilo kwani kuna hujuma ambazo zinafanywa kukidhoofisha chama. Lakini tunasubiri uamuzi wa polisi kama kutakuwa na dhamana au la dhidi ya mgombea wetu ubunge na wanachama wetu 15," alisema.


**THE COMPANIES ACT, CAP 212 (R.E 2002)**

**BBMG COMMERCIAL & TRADING COMP. LIMITED**

**NOTICE OF RESOLUTION TO CEASE THE BUSINESS IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**NOTICE** is hereby given to the general public that by special resolution dated 16th June, 2020, **BBMG COMMERCIAL & TRADING COMP. LIMITED** resolved to cease the place of business and strike off the said company.

**FURTHER NOTICE THAT I,** EDRICK LUIMUKA, of New Bagamoyo Road, 4th Floor Letsya Tower, Plot 59c, Kijitonyama, Dar Es Salaam,was appointed for the purpose of ceasing the business of **BBMG COMMERCIAL & TRADING COMP. LIMITED.**

**TAKE NOTICE** that all the creditors are hereby requested to furnish the liquidator with full details of their claims against the company at the address below within fourteen days (14 days) from the date this notice has been published.

Dated and Signed this 10th day of August, 2020

**EDRICK LUIMUKA, Liquidator**
**ADDRESS:**
**NEW BAGAMOYO ROAD,**
**4TH FLOOR LETSYA TOWER,**
**PLOT 59C, KIJITONYAMA,**
**DAR ES SALAAM**

**THE COMPANIES ACT, CAP 212 (R.E 2002)**

**HYSEAS INTERNATIONAL INVESTMENT (T) LIMITED**

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP THE COMPANY VOLUNTARILY BY MEMBERS**

**NOTICE** is hereby given to the general public that by special resolution dated 30th January, 2019, **HYSEAS INTERNATIONAL INVESTMENT (T) LIMITED** resolved to wind up the company voluntarily by members.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT I,** Edrick Luimuka, of P.O BOX 42450, Ubungo, Dar es Salaam, was appointed for the purpose of winding up **HYSEAS INTERNATIONAL INVESTMENT (T) LIMITED.**

**TAKE NOTICE** that all the creditors are hereby requested to furnish the liquidator with full details of their claims against the company at the address below within fourteen days (14 days) from the date this notice has been published.

Dated and Signed this 12th day of August, 2020

**Edrick Luimuka, Liquidator**
**ADDRESS:**
**Mkapa Export, External**
**Ubungo, Dar es Salaam**

HABARI KITAIFA

# Saruji ya Tanzania yapata soko EAC, SADC

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA imepata neema ya soko kubwa la saruji kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alisema hayo jana alipotembelea kiwanda cha kuzalisha saruji cha Camel, kilichoko Mbagala, jijini Dar es Salaam.

Bashungwa yuko kwenye ziara ya kukagua hali ya uzalishaji kwenye viwanda vya saruji kuangalia changamoto na kuzitatua baada ya nchi kadhaa kutaka kununua saruji ya Tanzania.

Alisema Tanzania ina viwanda 13 vya saruji ambavyo vina uwezo wa kuzalisha tani milioni 10.6 kwa mwaka lakini mahitaji ya ndani kwa mwaka yanafikia tani milioni sita tu, hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha ziada ya kuuza nje.

"Kwenye uzalishaji viwandani tuko vizuri sana na tunazidi kufanikiwa na ndiyo sababu wenzetu wameona nchini kwetu kuna fursa ya kununua saruji kwa sababu kwa sasa tuna ziada ya kuuza nje. Tunamshukuru Rais (John) Magufuli kwa maono yake makubwa kwenye sekta hii," alisema.

Bashungwa alisema hatua ya nchi hizo kuiomba Tanzania izalishe saruji kwa wingi ili zije kununua ni jambo la kujivunia.

"Kutokana na fursa hii, Wizara tutaenda kila kiwanda kuangalia wanapokwama na tuwasaidie wasonge mbele kwasababu tukiongeza uzalishaji tutaongeza pia ajira kwa vijana wetu hapa nchini," aliongeza Bashungwa.

Alisema kiwanda hicho kimejitahidi kuwekeza kwenye teknolojia ya kisasa na kuzalisha saruji nyingi na amewashauri watafute teknolojia zaidi kwaajili ya kujipanua zaidi ya Mbagala.

Waziri Bashungwa alisema serikali inataka kuona viwanda vya saruji vinajipanua na kujenga vingine kwenye mikoa ya kati na ile ya Kanda ya Ziwa ili kuachana na usafirishaji wa bidhaa hiyo kwa umbali mrefu.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe, kukaa na wenye viwanda ili kuangalia wanavyoweza kuwekeza mikoa mingine na kama kutakuwa na changamoto wazitatue.

"Wizara inataka kujua mnataka nini na kwa sababu nia yetu ni kuona viwanda vinajengwa mikoa ya kanda ya kati na Kanda ya Ziwa tutawasaidia kutatua changamoto mtakazotuambia," alisema

Meneja Mkuu wa Camel Cement, Sundarraj Rajagopal, alisema wanaweza kuongeza uzalishaji kama watawekewa mazingira mazuri zaidi kama upatikanaji wa rasilimali za kuzalisha bidhaa hiyo.

Alisema serikali kupitia wizara hiyo itawasaidia sehemu ambayo wanaweza kupata kwa urahisi rasilimali ya 'limestone' na 'crinker' ili waongeze uzalishaji na bei ya bidhaa hiyo itashuka.



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (katikati), akifurahia jambo na Meneja Mkuu wa kiwanda cha saruji cha Camel cha Mbagala jijini Dar es salaam, Sundarraj Rajagopal (kulia), alipofanya ziara ya kuangalia changamoto za kiwanda hicho kwenye mwendelezo wa ziara zake za kutembelea viwanda vya saruji. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ujenzi kiwanda waleta neema kwa wafugaji

**Na Mwandishi Wetu, KIBAHA**

KILIO cha muda mrefu cha wafugaji kukosa soko la uhakika la mifugo yao kimefika mwisho baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kiwanda cha Tanchoice, Kibaha mkoani Pwani.

Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuchinja mbuzi na kondoo 6, 000 na ng'ombe 1,000 kwa siku, kimeanza uzalishaji kinasafirisha nyama ya mbuzi, ng'ombe na kondoo Kuwait na Oman.

Sambamba na hilo kimewezesha ajira mpya 240 za vijana wa Kitanzania na ajira hizo zinatarajiwa kuongezeka hadi kufikia 500

Akizungumza jana baada ya kushuhudia uchinjaji mifugo kwa mara ya kwanza kwenye kiwanda hicho, Waziri wa Mifugo, Luhaga Mpina, alisema kuanza kufanya kazi kwa kiwanda hicho, ni moja ya mafanikio makubwa ya serikali katika kuongeza thamani ya mifugo na kuwezesha kukua kwa biashara ya mifugo nchini.

Waziri Mpina alisema kuanza kufanya kazi kwa kiwanda hicho kutawezesha ongezeko la uzalishaji wa mifugo kwa wafugaji sambamba na kupanuka kwa soko la mifugo. Alisema wafugaji sasa watakuwa na soko la uhakika la kuuza mifugo na kuwataka kuongeza kasi ya uzalishaji na kuchangamkia fursa ya ujio wa kiwanda hicho.

Mpina aliwapongeza wamiliki wa kiwanda cha Tanchoice kwa jitihada kubwa walizofanya za kuunga mkono serikali kufikia azma yake ya nchi ya viwanda na kuelezea kufurahishwa kwake na teknolojia kubwa iliyotumika kusimika mitambo ya uchinjaji mifugo pamoja na kiwango cha juu cha usafi wa mazingira katika kuzalisha nyama bora.

Pia Waziri Mpina alimhakikishia mwekezaji huyo kuwa serikali iko macho na kwamba itaendelea kutoa ushirikiano wote katika kuwezesha kiwanda hicho kufanya kazi vizuri na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Ile ndoto yenu Watanzania ambayo mliisubiri kwa muda mrefu sasa imetimia. Baadhi ya watu walidhani ni maneno tuu sasa kiwanda kikubwa kimeanza kufanya kazi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TANCHOICE, Rashid Abdilah, aliishukuru serikali kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara hasa kudhibiti uingiziaji holela wa mazao ya mifugo nchini jambo lililowezesha kuamua kuja kujenga kiwanda hicho kikubwa na cha kwanza katika nchi za Afrika Mashariki na Kati.

Rashid alisema kwa sasa kiwanda hicho tayari kimepata vibali vyote muhimu vikiwamo vya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Halal, Bodi ya Nyama Tanzania na cha Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania tayari kwa kuanza kusafirisha nyama katika nchi za Kuwait na Omani.

Msajili wa Bodi ya Nyama, Imani Sichalwe, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa wataendelea kusimamia kikamilifu wawekezaji hao ili kuhakikisha viwanda vingi zaidi vinaanzishwa nchini na kuwezesha kupatikana soko la uhakika la mifugo na kukuza uchumi kupitia sekta ya mifugo.

Pia alisema Bodi ya Nyama itaendelea kushirikiana na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) ili kupata uhakika wa ndege ya kusafirisha nyama kwa haraka kwenda kwenye masoko makubwa duniani.

Wakala wa kwanza kuleta mifugo katika kiwanda hicho, Tawala Kamoga, alipongeza jitahada za serikali kuwaletea kiwanda hicho. Kabla ya kiwanda hicho, alisema walikuwa wakilamizika kuuza nje ya nchi huku mifugo yao ikidhoofika na kuuzwa kwa bei ndogo kutokana na safari ndefu nje ya nchi pamoja na kutapeliwa.

# Benki tatu zaungana kuwa moja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI za Mwanga Community, Hakika Microfinance na EFC Tanzania Microfinance zimeungana na kuwa benki moja ijulikanayo kama Mwanga Hakika Microfiance Bank Ltd.

Muunganiko huo umefanyika baada ya kuridhiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Tume ya Ushindani (FCC) na kuundwa kwa benki moja yenye thamani ya billion 40.5 ya mali.

Muungano huo ulizinduliwa rasmi katika hafla iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam iliyohudhuriwa na Naibu Gavana wa BoT, Dk. Bernard Kibesse na kushuhudiwa na wadau mbalimbali kutoka sekta ya fedha.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki hiyo, Ridhuan Mringo, alisema muungano huo ni muhimu katika kuunda benki imara inayoweza kutoa huduma zenye viwango kwa wateja zenye kuzingatia unafuu na teknolojia za kisasa.

"Tunaamini kwamba huu ni muda wa kuimarisha sekta ya kibenki na hii imejidhihirisha kwa baadhi ya benki ambazo ziliamua kuungana na kuunda benki moja imara. Tumeamua kuungana ili kutengeneza benki kubwa na imara ambayo itasaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa biashara yetu," alisema Mringo.

Aliongeza kuwa kupitia benki hiyo, wateja watapata huduma zilizoboreshwa zaidi na bidhaa zenye ubunifu katika mikopo na uhifadhi wa fedha ambazo zitakuwa nafuu na za haraka.

"Kuanzia sasa mahitaji ya kila siku ya kibenki ya wateja wetu yatatimizwa na benki hii mpya. Tunatarajia kukua kwa makusanyo ya akaunti za wateja kwa sababu benki hii itakuwa suluhisho la mahitaji mbalimbali ya kifedha," alisema.

Kupitia muungano huo, benki mpya itakuwa na mtandao mkubwa wa usambazaji huduma ikiwa na matawi saba ambayo yatakuhudumia wateja 105,000 nchi nzima.

Dk. Kibesse alipongeza hatua iliyochukuliwa na benki hizo na kwamba itasaidia katika uimarishaji wa sekta ya kibenki kwa kuhakikisha watu ambao hawajafikiwa na huduma wanapata nafasi hiyo.

Pia alisema itasaidia katika kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuwa benki hiyo itakuwa na wigo mpana wa kutoa mikopo hasa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati jambo litakalochangia kuleta ujumuishwaji wa uchumi.

HABARI KITAIFA




Mkurugenzi wa Dijitali na Huduma za Ziada Vodacom Tanzania, Nguvu Kamando, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu shindano la kuibua vijana wa Kitanzania wenye wazo la ubunifu wa teknolojia, ambapo siku ya jumanne watatangaza washindi watatu walioshinda shindano hilo. Zaidi ya kampuni chipukizi 500, waliwasilisha mawazo bunifu kutoka kote nchini. Kulia ni Mwendesha Mradi Mwandamizi wa SmartCode, Isaack Shayo na Meneja Mradi huo, Sharron Nsule. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM kupuliza kipenga kampeni urais Agosti 29

**Na Romana Mallya**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, amesema mgombea wa urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli, atazindua kampeni zake Agosti 29, mwaka huu jijini Dodoma.

Polepole alibainisha hayo jana kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ambako leo kunafanyika tamasha la uzinduzi wa nyimbo za kampeni za CCM katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari uwanjani huko, Polepole alisema kama sehemu ya kuheshimisha uamuzi wa Rais Magufuli kuhamia Dodoma, imempendeza kampeni za kuwania urais zizinduliwe jijini Dodoma.

Alisema CCM kina shughuli kadhaa za ndani kama sehemu ya kujipanga kuelekea katika kampeni kuanzia ngazi ya kata, majimbo, wilaya, mikoa na zinazoratibiwa ndani na nje ya chama.

Alisema shughuli hizo wamezifanya ziwe za ndani na siyo za hadhara, macho na masikio ya wengi yakisubiri hatima ya makada wa chama hicho walioomba ridhaa ya kuteuliwa kuwania ubunge na uwakilishi.

Kuhusu tamasha la leo, Polepole alisema kutakuwa na wasanii wa sekta mbalimbali 300 wakiwamo waimbaji wa muziki wa dansi, wachekeshaji na waigizaji wa filamu.

Alisema wasanii hao wamejitoa wenyewe na wanaunga mkono chama na serikali kwa kueleza kwa lugha ya sanaa mambo ambayo Rais Magufuli na serikali wamekuwa wakiyafanya kwa miaka mitano ya uongozi wake.

## NGO zafunga ofisi kisa kukosa fedha

**Na Mwandishi Wetu,** SHINYANGA

OFISI ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGO) imebaini kasoro mbalimbali katika baadhi ya asasi hizo mkoani Shinyanga ikiwamo baadhi kutokufanya kazi licha ya kuwa na usajili.

Akizungumza jana wakati wa kikao cha majumuisho na mashirika hayo, Jaina Said kutoka Ofisi ya Msajili wa NGO nchini, alisema baadhi ya asasi hizo mkoani hapa hazifanyi kazi kwa kisingizio cha kukosa ufadhili.

Kutokana na hali hiyo, alionya kuwa huo ni upungufu wa kisheria kwa kuwa hakuna NGO inayosajiliwa na serikali kwa lengo la kupatiwa ufadhili.

"Unaposajili shirika hakuna mahali sheria inatamka kuwa utakuwa na ufadhili ila unapokamilisha usajili unatakiwa kuanza kazi kwa bajeti ndogo unayokuwa nayo kwa kuwa mashirika yanasajiliwa kwa lengo la kutoa huduma kwa jamii na mfadhili hawezi kukuona ukiwa nyumbani kwako," alisema.

Mbali na sababu hiyo, alisema kasoro nyingine aliyobaini ni baadhi ya asasi hizo kushindwa kuwasilisha taarifa za mwaka. Aliutaja mwaka wa NGO kuwa ni Januari hadi Desemba kama Fomu Na. 14 iliyoko katika tovuti ya msajili inavyotaka mashirika yote binafsi kuwasilisha taarifa za robo mwaka lakini pia fomu ya NGO namba 10 inayotaka kuwasilisha taarifa ya mwaka pamoja na viambatanisho vinavyoelekezwa na fomu hiyo.

Ofisa huyo pia alisema mashirika mengi yamekuwa yakifanya mabadiliko mbalimbali ikiwamo bodi na eneo la ofisi bila kutoa taarifa kwa msajili wa mashirika kwa kuwa shirika linaposajiliwa linakuwa na wasifu wa viongozi, mtaa na bodi hivyo kunapotokea mabadiliko hayo ni lazima kutoa taarifa.

Naye Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Shinyanga, Beda Chamatata, aliyataka mashirika mkoani Shinyanga kuhakikisha yanafanya kazi kwa ukaribu na serikali mkoani hapa ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu sughuli za mashirika hayo.

Aidha, Chamatata aliyataka mashirika hayo kuunda chombo cha pamoja kitakachoyawezesha mashirika kutambuana na kujua maeneo ya kufanyia kazi kwa lengo la kuondoa kurudia kazi zile zile japo utekelezaji ni wa mashirika tofauti.

Kaimu Meneja wa TRA Mkoani Shinyanga alisema maeneo ya NGO yanayosamehewa kodi yanapaswa kutambua kuwa kodi ya mapato katika mishahara ya viongozi na watumishi ni lazima kulipa mapato kama ilivyo kwa watumishi wengine katika maeneo yao ya kazi.

# TCRA yashusha rungu vyombo vya habari

**Na Mary Geofrey**

KAMATI ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imevishushia rungu vyombo vya habari vya utangazaji tisa kutokana na makosa mbalimbali ya ukiukaji wa kanuni za utangazaji wa redio na televisheni na maudhui ya mitandaoni.

Watoa huduma waliokumbwa na rungu hilo ni Carry Mastory Media Ltd, Triple A FM, CG FM; Wasafi Media Online TV; Clouds FM Radio; Radio One; Radio Free Africa; Kiss FM Radio; na Abood FM Radio. Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui wa TCRA, Joseph Mapunda, alisoma uamuzi wa kamati hiyo jana jijini Dar es Salaam, mbele ya waandishi wa habari.

Mapunda alitaja adhabu zilizotolewa kwa vyombo hivyo ni kufungiwa kwa kipindi cha Jahazi cha Clouds Redio, vituo viwili vya redio kutozwa faini ya Sh. milioni tano kila kimoja, vingine kupewa onyo kali na kuwa chini ya usimamizi wa mamlaka.

Alikitaja kituo cha redio cha Clouds Entertainment kufungiwa kutangaza kipindi chake cha Jahazi kwa kosa kwa kutangaza kipindi chenye maudhui ya lugha isiyo na staha na yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono, kujichua au kupiga punyeto.

Alisema Clouds Radio walitenda kosa hilo, Juni 26, mwaka huu la kukiuka kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018 Na. 11 (1) (c), 12(1) (a), (d) na 14 (a), (b) na (c).

Alisema Kwa mujibu wa Kifungu cha 28 (1) (b) na (d) cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172, Marejeo ya Mwaka 2017, Kamati ya Maudhui iliamua kutoa adhabu ya kukifungia kipindi cha Jahazi na kutorusha kipindi kingine chenye maudhui kama hayo kwa sababu kituo hicho kimekuwa kikionywa mara kwa mara. Alitaja kituo kingine cha Wasafi Media Online TV, kupitia Chaneli yake ya YouTube, kilitozwa faini ya Sh. milioni tano kwa kuchapisha na kutangaza maudhui yenye lugha ya kuwakebehi wagombea mbalimbali ambao walikwenda kuchukua fomu za kugombea viti vya udiwani na ubunge na kuwafanyia kampeni bila kuzingatia mizania, kinyume cha Kanuni Na. 7(1) (a) na (b); 12 (b). Aidha kituo hicho pia kilitozwa faini ya Sh. milioni tano na kupewa onyo kali kwa kosa la kurusha matangazo yenye maudhui yasiyo na maadili ya utangazaji kwa kuhamasisha ufanyaji mapenzi. Mapunda alivitaja vituo vingine kuwa ni Carry Mastory Media Ltd, kilichotozwa faini ya Sh. milioni tano na onyo kali kwa kuchapisha habari za kuchochea mapenzi kinyume cha maumbile.

Alikitaja kituo kingine cha Triple A FM kilichotozwa faini ya Sh. milioni tano na kuwa chini ya uangalizi wa TCRA kwa miezi sita na kituo cha CG FM kwa kukiuka agizo la Serikali na kutozingatia mizani ya habari, wamewekwa chini ya uangalizi kwa miezi tisa.

Mapunda alivitaja vituo vingine vinne vya Radio One Stereo, Radio Free Africa, Kiss FM Radio na Abood FM Radio kwa kurusha maudhui bila kuzingatia mizania ya habari walipokuwa wakimhoji Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA),Tundu Lissu, kuhusu viongozi wa chama hicho kutoshiriki katika kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu, Hayati Benjamin Mkapa. Mapunda alisema maudhui hayo yalirushwa kupitia vipindi vya Amka na BBC, kinachorushwa na vituo hivyo, kinyume na Kanuni Na 15(2) (b) na (c) Na. 16 za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Alisema baada ya kusikiliza utetezi huo, walitoa adhabu ya onyo kwa Redio One Stereo na Redio Free Africa na kuwekwa chini ya uangalizi kwa miezi mitatu.

Alisema Kiss FM, waliwashauri kuendelea kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya uandishi na utangazaji wa habari katika kazi zao na Redio Abood FM ilipewa onyo kali na kuwekwa chini ya uangalizi kwa miezi sita.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF ina maswali ya kujibu hukumu Morrison, Yanga

**KAMATI** ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), Jumatano wiki hii ilimtangaza kiungo mshambuliaji raia wa Ghana, Bernard Morrison, kuwa mshindi katika kesi yake dhidi ya klabu yake ya zamani, Yanga, iliyovuta hisia kubwa kwa mashabiki, wadau wa soka na Watanzania kwa ujumla.

Katika kesi hiyo, mlalamikaji Morrison alikuwa alidai hana mkataba wa kuichezea Yanga baada ya ule wa awali wa miezi sita kumalizika na kwamba mkataba mpya wa miaka miwili unaoelezwa kuingia na klabu hiyo, si halali na kwamba saini yake ilighushiwa, suala ambalo tunaamini Jeshi la Polisi bila shaka lilihusishwa na kuweka majibu ya uchunguzi wake mezani.

Kamati hiyo ikiwa chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala ililazimika kujifungia kwa siku tatu kutafuta ukweli kwa kupitia nyaraka mbalimbali na mkataba huo pamoja na kuwahoji wahusika kuanzia Agosti 10 kabla ya Jumatano jioni kutoa hukumu kwa kumtangaza Morrison mshindi.

Mwanjala alimtangaza Morrison mshinda kwa kile alichoeleza mkataba kati yake na Yanga kuwa na upungufu mkubwa upande wa tarehe ambapo kuna sehemu ilionyesha amesaini Machi 20 huku chini ukionyesha kasaini Julai 15, 2020.

Lingine lililochangia kumpa Morrison ushindi alisema kuwa ni ukurasa wa saini kwenye mkataba unaonyesha kuna upungufu katika sehemu ya saini ambayo imefutwa kwa kalamu jambo ambalo linaonyesha kulikuwa kuna tatizo kwenye masuala ya mkataba. Hata hivyo, swali ambalo bado mashabiki na wadau wa soka wanataka kulijua, ni vipengele vilivyompa Morrison ushindi kutoka kesi ya kughushi ambayo walitarajia kupata majibu ya Jeshi la Polisi, lakini wakashangaa akitangazwa kushinda kwa kasoro za tarehe kwenye mkataba na kasoro katika ukurasa wa saini, ambazo zinaelezwa kufutwa kwa kalamu.

Swali lingine linaloleta ukakasi kwa wadau wa soka, ni vipi saini inaweza kuondoa uhalali wa mkataba huo kama mambo mengine ya msingi yalikuwapo kwenye mkataba yalizingatiwa?

Lakini pia kama suala lilikuwa tu upungufu ya saini kukatwa na tofauti ya tarehe, je, walipaswa kutumia siku tatu kulibaini hilo? Na mkataba huo ulishapokelewa TFF? Kama ndivyo, kwa nini siku zote hizo isiwarejeshee wahusika (pande mbili) kurekebisha kwanza upungufu yaliyopo. Tayari kumezuka minong'ono mingi kuwa kuna upande umebebwa ili kumaliza suala hilo kiutu uzima kwa madai kuwa endapo ingeamuliwa kwa kufuata kesi iliyokuwa mbele yao, ya kughushi saini kuna upande ungeumia vibaya.

Pia wapo wanaoamini kwamba ushindi wa Morrison ulitolewa ili kuibeba Yanga na kufunika suala la kughushi wakiamini huenda ni kweli ilighushi saini ya mchezaji huyo, huku baadhi wakiamini kiungo mshambuliaji huyo ushindi wake umetolewa ili kuibeba Simba ambayo ilishatangaza kumsajili.

Madai na minong'ono yote inatokana na jinsi wabobezi wa mambo ya sheria, wanavyochambua upungufu mkubwa uliopo katika hukumu hiyo, wakiwa wanazingatia sababu zilizompa Morrison ushindi kwa kutazama kesi ya msingi iliyokuwa inasikilizwa ambayo ilikuwa ya kughushi.

Katika hili Nipashe hatuegemei upande wowote ule, bali lengo letu tunataka kuona haki inatendeka na ili ionekane inatendeka kweli, basi uchunguzi wa Jeshi la Polisi kuhusu usahihii wa saini ya Morrison uwekwe mezani, jambo ambalo tunaamini litaondoa ukakasi katika sakata hilo na soka letu ambalo limeanza kupiga hatua. Kwa kuwa milango ipo wazi kwa Yanga kuomba kupitiwa upya kwa mwenendo mzima wa kesi hiyo, tunaona ni bora ikafanya hivyo kama tu inauhakika na madai yao, kabla ya uamuzi wao wa kwenda chombo cha juu, Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Mambo ya Michezo, CAS.

Kama ambavyo wakati Mwanjala akisoma hukumu hiyo alisema, walikuwa makini na kamati yake katika kufuata haki, Nipashe tunaamini, umakini zaidi utatumika kupitia upya mwendo wa kesi hiyo endapo Yanga itaridhia kufanya hivyo, jambo ambalo litajibu maswali yanayowatesa wadau wa soka na kila upande kuridhika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Wajinga ndiwo waliwao!

**NAAM,** wajinga ndiwo wanaopumbazwa au kuliwa. Hii ni methali ya kutumiwa kumpigia mfano mtu ambaye ameishia kudanganywa kwa njia inayoonekana kuwa rahisi sana.

Agosti Mosi, 2020, niliandika kwenye gazeti hili kuishauri Yanga iachane na mchezaji Bernard Morrison iliyemsajili kutoka Ghana nikimlinganisha na kirusi, yaani kiini kinachosababisha ugonjwa. Niliitahadharisha Yanga iachane na Bernard ili asiwaambukize virusi wachezaji aliowakuta klabuni.

Kwa kuwa viongozi wa Yanga hawakunielewa au walinifanya zumbukuku, yaani mtu asiye na uwezo wa kufahamu undani wa mambo, wakaendelea kumng'ang'ania Morrison, naye akazidi kuvimba kichwa. Akakimbilia Simba na kusajiliwa kimya kimya!

Songombingo (jambo lenye mazonge mengi kiasi kwamba mtu hajui aanze vipi ili kulifanikisha) likaanzia hapo. Kwanza Morrison alikiri kushawishiwa na Simba ili ajiunge nao kwa fedha zaidi ya alizoahidiwa na Yanga. Simba walipokanusha, Morrison akanyamaza kana kwamba hakuna kinachoendelea kumbe mambo yalikuwa yakifanywa kimya kimya! Wahenga walisema: "Kimya kimya si ujinga ni maneno kupeleleza." Umwonapo mtu ametulia tuli (bila ya kutikisika) huwa si mjinga bali anachunguza mambo yalivyo. Methali hii yatukumbusha umuhimu wa kuchunguza au kupeleleza mambo kabla ya kufanya uamuzi au kuyadakia.

Ilisemwa na wahenga kuwa "Fedha ilivunja nguu, milima ikalala." Maana yake pesa zina uwezo wa kuivunja milima na vilima. Methali hii hutumiwa kupigia mfano uwezo wa fedha. Mtu akiwa na pesa anaweza kufanikiwa kufanya mambo ambayo asingeweza kuyafanya wala kudhania kuyafanya.

Simba ilimsainisha Morrison kimya kimya bila kutangaza huku akiendeleza ujeuri wake kwa timu iliyomleta Tanzania , Yanga. Baada ya Simba kupekenyua (kitendo cha kutoa kitu sehemu ya mbali kilipofichwa au kuwekwa) ikatangaza kumsajili Morrison na kuweka picha za tukio hilo mitandaoni wakati mchezaji huyo akitia saini akiwa kavaa jezi ya klabu yake mpya Simba!

Yanga wakashtuka. "Khaa! Mchezaji tumlete sisi, leo Simba wamchukue kirahisi namna hiyo? Tutakutana TFF ndio tutajua mbichi na mbovu ..." Wapi bwana. Kumbe Simba walishafanya uchunguzi na kung'amua kuwa vyovyote itakavyokuwa, Morrison ni mchezaji wao ... na imekuwa hivyo! Ukimya wa TFF una maana gani?

Pamoja na yote hayo, kuna maswali mengi yanayopaswa kujibiwa na Kamati ya Sheria na Hadhi ya Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania, (TFF). Mchezaji anadai Yanga ilighushi saini yake na kukana kuutambua mkataba wake na Yanga.

Kamati ikaamua kupeleka suala hilo Polisi ili lifanyiwe uchunguzi. Hata Polisi ilipomaliza uchunguzi wake na kuwasilisha kwa kamati husika, ilishindwa kuweka wazi kilichogunduliwa na Polisi. Matokeo ya uchunguzi ule yangetosha kumaliza mvutano kati ya Morrison na Yanga.

Ukimya wa kamati kutoweka wazi uchunguzi wa Polisi kuhusu saini ya Morrison kama ilighushiwa ama la una maana gani? Je, kamati hiyo ina wapenzi wengi zaidi wa timu moja kati ya Yanga na Simba ndo sababu kesi ya Yanga na Bernard imepigwa danadana? Au ni kile kinachoitwa 'damu ni nzito kuliko maji?'

Jambo lingine la kushangaza ni TFF kutofuatilia malalamiko ya Yanga kuishitaki Simba kumrubuni Morrison wakati akiwa na mkataba na Yanga. Yapo mambo mengi yaliyofanywa kinyume cha sheria na TFF kadhalika kamati yake, kuhusu mgogoro wa Yanga, Morrison na Simba.

Timu za Simba na Yanga zina mambo ya ajabu sana katika usajili wa wachezaji na hata vingozi wao. Hebu fikiri Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Senzo Mazingisa aliyesajiliwa kutoka Afrika Kusini anajiuzulu ghafla kisha anadaiwa kuajiriwa na Yanga haraka haraka. Inaonesha picha gani?

Wakati mwingine Simba na Yanga hufanyiana mambo ya kitoto kwa kile wanachodai kukomoana kumbe wanajikomoa wenyewe ila hawajitambui! Wanaposajili wachezaji huweka majina yao hadharani hata kabla ya kuongea wala kuwasiliana nao! Upande mmoja ukipata habari hizo, huingilia kati na hapo hutokea mvutano kati yao. Kwa nini hawafanyi usajili wa kiungwana, kimya kimya na kutangaza wachezaji baada ya kukubaliana na kuwasajili? Tofauti na utaratibu huo ni ulimbukeni na matokeo yake kuna upande unamkosa mchezaji aliyekusudiwa.

Tunarudi kwa mchezaji Bernard Morrison. Huyu alicheza mpira sehemu mbalimbali duniani akiishia Afrika Kusini kabla ya Senzo Mazingisa kujiunga na Simba. Kwa hiyo anafahamu visa vya Morrison vilivyosababisha afukuzwe humo nchini. Kwa sababu hizo, nadhani, narudia tena, nadhani aliwashauri viongozi wa Simba kutomsajili kutokana na tabia zake, lakini huenda alipuuzwa ... akasajiliwa. Je, haiwezekani alipoona kapuuzwa, aliamua kujiuzulu na kujiunga na wapinzani wao wa jadi, Yanga?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara ya Mwalimu (MCB), Richard Makungwa (kushoto), akizungumza kwenye Mkutano Mkuu wa Nne wa Wanahisa wa benki hiyo, kwenye ukumbi wa Isike Mwanakiyungi, mjini Tabora juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbarawa amtaka mkandarasi kukamilisha mradi kwa wakati

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amemwagiza mkandarasi anayetekeleza mradi wa maji kutoka Shinyanga hadi Kata ya Masengwa, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, kuukamilisha ifikapo mwezi ujao kama mkataba unavyoelekeza.

Prof. Mbarawa alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua mradi huo unaotekelezwa na kampuni ya Emirates Builders ya Dar es Salaam kuwa matarajio makubwa kwa wananchi wa kata hiyo ya Masengwa ni kuondokana na ukosefu wa maji. Alisema miradi mingi ya maji inayotekelezwa na makandarasi imekuwa na changamoto ya kutokamilika kwa wakati pamoja na kutumia gharama kubwa tofauti na ile ambayo inatekelezwa na wataalam wa ndani.

"Ninaagiza mradi huu ukamilike ndani ya mwezi Septemba. Wananchi wamekuwa wakipata adha kubwa ya maji, ilhali mradi upo. Iwapo utashindwa kukamilisha kwa wakati tutaleta wahandisi wa wizara, watakamilisha na hutapewa kazi yoyote ndani ya Wizara ya Maji," alisema Mbarawa.

Naye msimamizi wa mradi huo, Mhandisi Saidi Msangi, kutoka kampuni ya Emirates, aliahidi kutekeleza agizo hilo na kubainisha kuwa kabla ya Septemba 27, mwaka huu, mradi huo utakuwa umekamilika.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema kutokana na kauli ya mkandarasi huyo kuwa atakuwa amekamilisha mradi katika muda alioutaja, atahakikisha anaufuatilia kwa ukaribu ili kuona utekelezaji wake na kujengwa kwa kiwango kinachostahili.

Katika hatua nyingine, Waziri Mbarawa alikagua utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) katika Kata za Ngongwa na Kitwana, Halmashauri ya mji wa Kahama na kupogeza hatua ambayo miradi hiyo imefikia ambayo inatekelezwa kwa kutumia 'Force Account'.

Akizungumzia ujenzi wa miradi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa SHUWASA, Flaviana Kifizi, alisema miradi hiyo imekamilika kwa asilimia kubwa na sasa wanasubiri kiasi Sh. milioni 80 kwa ajili ya kuchimba mitaro ya kulaza mabomba.

Waziri Mbarawa alimhakikishia fedha hizo zitafika ndani ya wiki mbili, ili kukamilisha miradi hiyo na kuhudumia wananchi.

# Stadi za maisha chachu ya kujitambua

**Na Julieth Mkireri,**
BAGAMOYO

IMEELEZWA kuwa kukosekana kwa stadi za maisha kwa wanafunzi kumesababisha kuwa na jamii ya watu wasiojitambua.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni mjini hapa na Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Ndoa na Malezi kwa Watoto Tanzania (TaMCare), Mchungaji Dk. Enock Mlyuka, wakati akitoa mafunzo ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Bagamoyo.

Dk. Mlyuka ambaye ni Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na mwanataaluma, alisema stadi za maisha ni muhimu kwa vijana ili kuandaa taifa lililo bora na kuwa na raia raia wema wenye kujitambua.

"Wazazi wengi wanalipa ada kwa watoto wao ili wasome lakini hawana muda wa kuwafuatilia na kuongea nao.

Yanayoendelea maishani yanatokana na makuzi, hivyo elimu inatakiwa kwenda sambamba na nidhamu kwa vijana." alisema Dk. Mlyuka.

Alisema stadi za maisha zinawasaidia vijana kujitambua, kuwajibika na kuwa na maarifa ya kukabiliana na changamoto watakazokutana nazo kwenye maisha.

"Kuna vijana wengi walioshindwa kutumia vizuri muda wao wakiwa shuleni, jambo ambalo limesababisha kuwa na maisha yasiyo na picha nzuri. Kijana anatakiwa kuwa na utaratibu mzuri wa kujisomea akiwa shule na hii itamsaidia kutengeneza maisha ya baadaye," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Bagamoyo, Khalfan Milongo, aliishukuru TaMCare kwa mafunzo hayo ambayo alisema yamewakumbusha mambo muhimu ikiwa ni pamoja na kuzingatia muda wakiwa shuleni.

Kiranja Mkuu wa Shule hiyo, Hamis Wambura, alisema mafunzo waliyopatiwa yamewafungulia ukurasa mpya wa kufanya mabadiliko hususani katika kipindi ambacho wako shuleni na kwamba watazingatia maelekezo waliyopewa ili kutengeneza maisha yao ya baadaye.

Naye Dada Mkuu wa Shule hiyo, Iotsam Hemed, alisema hawakuwahi kupatiwa mafunzo kama hayo na kwamba elimu hiyo wataitumia kuleta mabadiliko na kuwa na matumizi mazuri ya muda.

Pia aliahidi kufanya mkutano na wanafunzi wote wa shule hiyo ambao hawajanufaika na mafunzo hayo ili kuwashirikisha na kuleta mabadiliko chanya.

TaMCare inaendesha mafunzo shuleni na kwa jamii ambayo imekosa stadi za maisha ili kuifanya iwe na mabadiliko na kutambua namna ya kukabiliana na changamoto inazokumbana nazo.

# Waliosoma nje kukutanishwa Dar es Salaam

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI 400 waliosoma vyuo vikuu mbalimbali nje ya nchi, watakutanishwa katika mahafali ambayo yanatarajiwa kuwa daraja la kupata fursa mbalimbali za uwekezaji na namna wanavyoweza kutumia ujuzi wao kujiajiri na kuajiri vijana wenzao.

Mgurugenzi wa Global Education Link (GEL), taasisi inayowaunganisha wanafunzi na vyuo vikuu nje ya nchi, Abdulmalik Mollel, alisema hayo jana wakati akizungumzia mahafali hayo yanayotarajiwa kufanyika Septemba 19, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Alisema lengo la mahafali hayo ni kuhakikisha wanafunzi Watanzania waliosoma nje ya nchi, hawarudi kimya kimya na kinyonge kwa kuwa wao ni wazalendo walioamua kuacha fursa zilizoko huko baada ya masomo yao na kurejea kuijenga nchi yao. Mollel alisema wahitimu hao waliaminiwa na taifa na ndiyo sababu walipewa visa za kwenda kusoma nje ya nchi kwa ajili ya manufaa yao, familia zao na nchi yao, hivyo kurudi kwao ni kurejesha furaha nyumbani kwa sababau wanatarajiwa kutoa mchango mkubwa kwa nchi.

Alisema GEL itawakutanisha wanafunzi hao kwa ajili ya kujenga mtandao na taasisi na watu mbalimbali nchini baada ya kukaa nje ya nchi kwa muda mrefu ambako walishajenga aina nyingine ya maisha.

"Mfano mtoto ameenda huko akiwa na miaka 17. Amekaa huko miaka minne au sita anarudi amekuwa mtu mzima amekuta mambo mapya. Sasa akifika akikosa timu kama aliyokuwa nayo kule, anakata tamaa. Kitendo cha kumkutanisha mtu aliyekuwa Uingereza, India, China, Canada au Afrika Kusini kwenye jengo moja ni jambo kubwa sana na la msingi," alisema Mollel.

Aidha, Mollel alisema wanafunzi hao wakikutanishwa wataona kama milango ya maisha yao imefunguliwa kwa kuwa watatengeneza mtandao mpya na wenzao waliomaliza nao mwaka mmoja kwenye vyuo hivyo nje ya nchi kwa sababu awali hakukuwa na mahafali ya aina hiyo.

Kwa mujibu wa Mollel, mahafali hayo ni fursa kwa wahitimu hao kwani kuna kampuni mbalimbali ambazo zimetoka kwenye nchi ambazo wanafunzi hao walisoma ambazo zitakuwa zinatafuta wataalamu wa fani wanazozihitaji hivyo wakikutanishwa itakuwa na manufaa kwao.

"Kuna wawekezaji ambao wanatafuta watu waliosoma kwenye nchi zao angalau wenye kujua lugha zao kidogo sasa hii ni nafasi ya kuwaita hawa kwamba nani amewekeza nini na anahitaji vijana wataalamu, sasa ukiwakutanisha ni fursa kubwa sana kwa wawekezaji na vijana," alisema Mollel. Alisema kuna taasisi za serikali kama menejimenti ya utumishi wa umma na Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania (TaESA), wanahitaji rasilimali watu ambazo zipo lakini hakuna daraja lililowakutanisha, hivyo mahafali hayo ni daraja la kuwaunganisha wahitimu hao na taasisi hizo.

Taasisi hizo za serikali na za binafsi, alisema, zitakaposhiriki kwenye mahafali hayo, zitapata kujua orodha ya wanafunzi waliosoma fani mbalimbali wanazohitaji, hivyo kutengeneza daraja baina ya pande hizo mbili na kuondoa malalamiko kwamba kuna uhaba wa wataalamu na vijana kulalamikia tatizo la ajira.

## Waziri akosoa utendaji idara ardhi Nyang'hwale

**Na Mwandishi Wetu, NYANG'HWALE**

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameonesha kutoridhishwa na kasi ndogo ya upangaji na upimaji ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita.

Akiwa katika ziara ya kikazi kukagua utendaji kazi wa sekta ya ardhi kwenye halmashauri hiyo jana, Dk. Mabula alisema kasi ndogo ya upangaji na upimaji maeneo imeifanya halmashauri hiyo kutoa idadi ndogo ya hati za ardhi na hivyo kuikosesha serikali mapato yatokanayo na kodi ya pango la ardhi.

"Wilaya ya Nyang'hwale maeneo yake lazima yapangwe na kupimwa vizuri, hatuwezi kulialia, hii wilaya mpya iwe wilaya ya mfano kuepuka ujenzi holela," aliagiza.

Naibu waziri huyo pia aliiagiza ofisi ya ardhi Mkoa wa Geita kwenda na timu ya wataalamu katika halmashauri hiyo wiki ijayo kusaidia kupanga na kupima maeneo sambamba na kupitia upya ramani za wilaya hiyo ili kuwa na dira itakayokuza Mji wa Nyang'hwale. Dk. Mabula alielezwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, Mariam Chaurembo, kuwa idara ya ardhi kwenye halmashauri hiyo imekuwa na malalamiko mengi hasa kwenye kazi za upimaji maeneo aliyosema yanasababishwa na watumishi wa idara hiyo.

Alisema pamoja na juhudi zake kuhakikisha maeneo mengi katika wilaya hiyo yanapangwa na kupimwa, watumishi wa idara ya ardhi wamekuwa wasumbufu na wakati mwingine huondoka kituo cha kazi bila yeye kujua kwa kisingizo kuwa wako chini ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Dk. Mabula alimtaka Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nyang'hwale kuwawajibisha watumishi wote wa sekta ya ardhi watakaoonesha utovu wa nidhamu kwake na kusisitiza kuwa pamoja na wizara yake kuwa na mamlaka ya nidhamu na ajira kwa watumishi wa sekta hiyo, lakini hawaruhusiwi kuondoka kituo cha kazi bila mkurugenzi kujua.

Katika ziara yake ya kikazi Mkoa wa Geita, Naibu Waziri Mabula aliitembelea pia Halmashauri ya Mji wa Geita na kukagua Masijala ya Ardhi ambapo alionyesha pia kutoridhishwa na utunzaji wa nyaraka za ardhi alioueleza kuwa unaweza kusababisha migogoro ya ardhi.

# Bosi TARURA ambana mkandarasi

**Na Geofrey Kazaula, KALAMBO**

MTENDAJI Mkuu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA), Victor Seff, amemtaka Mkandarasi Mbuya's Contractors Company Limited, anayejenga barabara ya Mjini-Matai katika Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo mkoani Rukwa, kukamilisha mradi huo kwa wakati.

Kwa mujibu wa mkataba kati ya TARURA na mkandarasi huyo, mradi wa ujenzi wa barabara hiyo ambayo unatokana na ahadi za Rais John Magufuli, unatakiwa kukamilika Novemba 2, mwaka huu.

Seff alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua miradi ya barabara mkoani hapa akimtaka pia mkandarasi huyo kuhakikisha anazingatia viwango vya ubora katika kutekeleza mkataba huo. "Unatakiwa kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa wakati, lakini pia unazingatia viwango vinavyotakiwa, na mimi mwenyewe nitarudi hapa kujiridhisha," aliagiza.

Kiongozi huyo wa TARURA pia alitembelea miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja katika halmashauri mbalimbali za Mkoa wa Rukwa ikiwamo ya Nkasi ambayo alikagua miradi ya ujenzi wa barabara za lami katika Mji wa Namanyere zilizokamilika na zinazoendelea kujengwa.

Pia, alitembelea na kujionea hali ya Daraja la Kavunja lililoko Kijiji cha Kirando wilayani Nkasi na kubainisha kutoridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huo na jinsi ambavyo Ofisi ya Mratibu wa Mkoa wa Rukwa inavyoshughulikia vikwazo vilivyojitokeza za menejimenti ya mkataba na usanifu wa daraja hilo.

Alisema atatuma timu ya wataalamu kwenda kufuatilia utekelezaji wa mradi huo na kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua kutatua matatizo yaliyojitokeza. Akiwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, kiongozi huyo wa TARURA alizuru kwenye Daraja la Kankwale lililoko Kata ya Kankwale ambalo pia limeharibika kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na kusababisha kukatika kwa mawasiliano.

Seff aliagiza ujenzi wa daraja hilo uanze mara moja kwa kutumia fedha za mwaka huu wa fedha, ili kuhakikisha huduma za usafirishaji zinarejeshwa kwa wananchi.

Kaimu Mratibu wa TARURA Mkoa wa Rukwa, Selemani Mziray, alisema kuwa katika Mji wa Namanyere, ujenzi wa barabara za lami zinazotokana na ahadi za Rais unaendelea vizuri, akibainisha kuwa hadi sasa kilomita mbili zimekamilika na kilomita moja iko katika utekelezaji ikitarajiwa kukamilika Aosti 30 mwaka huu.

"Tunajitahidi ili kuhakikisha miradi hii inayotokana na ahadi za Rais inakamilika kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa ili wananchi wanufaike, alisema Mziray. Kabla ya kuhitimisha ziara yake mkoani Rukwa, Mtendaji Mkuu wa TARURA alifanya kikao kazi na mameneja wote wa TARURA walioko kwenye halmashauri zote za mkoa huo ili kutoa maelekezo na kujadili namna ya kuendelea kurejesha mawasiliano kwa maeneo yaliyoathiriwa na mvua.




Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfield (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 10 kwa Mkurugenzi wa Novefeed, Diana Orembe (kushoto), ambaye ni mmoja wa washindi watano wa shindano la ujasiriamali, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam, juzi. Katikati ni Mkuu wa Masoko wa benki hiyo, Desideria Mwegelo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki ya Walimu yaboresha huduma

**Na mwandishi wetu, TABORA**

BENKI ya Mwalimu, imewahimiza wanahisa wake na wananchi kutumia huduma za benki hiyo kwa kuwa inazidi kuimarisha miundombinu yake, ili kuwafikia wateja kwa urahisi zaidi nchi nzima.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano mkuu wa nne wa wanahisa wa benki hiyo uliofanyika Ukumbi wa Isike Mwanakiyungi mkoani Tabora juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa benki hiyo, Richard Makungwa, alisema benki itaendelea kuimarisha miundombinu yake ili kuweka mazingira mazuri ya biashara. Alisema mkakati uliopo sasa ni kuongeza matawi zaidi mbali na mawili yaliyoko Dar es Salaam, wakijipanga kufungua tawi la tatu jijini Dodoma kabla ya mwisho wa mwaka huu.

"Tuna huduma za Mwalimu Mobile. Vilevile, huduma ya Mwalimu Wakala ambayo mpaka sasa tuna mawakala wapatao 90 nchini. Wateja wetu wanaweza kupata huduma za ATM kupitia UMOJA Switch na wanaweza kuweka hela kupitia matawi yote ya TPB (Benki ya Posta) nchi nzima.

"Vilevile, tunatarajia kuanza kutoa VISA Card kwa wateja wetu kabla ya kufikia mwishoni mwa mwaka huu," alifafanua.

Alisema benki itaweka mazingira mazuri ya biashara ili walimu na wanahisa kwa ujumla kutumia huduma za benki hiyo katika kukata bima za mali na maisha yao kupitia benki hiyo ambayo sasa ni wakala wa bima.

Alisema kwa kufanya hivyo, wanahisa wote kwa ujumla wahamasike kutumia huduma za benki hiyo katika kufanyia shughuli zao zote za kifedha ili kuiwezesha benki kujiongezea mapato ili kuharakisha muda wa kutoa gawio kwa wanahisa.

"Benki pia inategemea mapato kutoka katika miamala mbalimbali kama kutoa pesa kwenye akaunti, kutuma fedha kupitia simu na kutuma pesa kwa mfumo wa kibenki na huduma za kibenki kupitia mawakala wetu," alisema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Deus Seif, alisema: "Walimu ninawaomba tutumie benki yetu, tutumie benki yetu, kuna sehemu tulizembea kidogo. "Wakati viongozi wetu wa Chama cha Walimu wanaanzisha hii benki, waliamini kwamba benki itakuwa na nguvu kuliko benki zote kwa sababu waliamini walimu wasiopungua 217,000 waliokuwapo Januari 2015, wote watafungua akaunti na kuitumia benki yao na sasa hivi ingekuwa benki kubwa na yenye nguvu licha ya vikwazo kadhaa, tujitahidi kutumia benki yetu."

Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema: "Mimi kama kiongozi wa walimu hapa Tanzania, nitumie nafasi hii kwanza kuwapongeza kwa uamuzi tuliofikia leo, lakini pia niendelee kuwasihi na kuwaomba wanahisa wenzangu ambao ni walimu tuendelee kuona umuhimu wa kuendelea kuithamini benki yetu na kadri bodi yetu itakavyotuelekeza wakati utakapofika tupeleke mishahara yetu kwenye Benki ya Mwalimu, tusisite kufanya hivyo."

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya benki hiyo, Herman Kessy, alisema mkutano huo wa wanahisa ni muhimu kwa kuwa pamoja na kupata taarifa rasmi kuhusu mwenendo na utendaji wa benki, pia umetoa nafasi ya kujadili mambo mbalimbali na kuyafanyia uamuzi.

"Nichukue fursa hii kuwashukuru sana, tena sana kwa kuniamini, mimi ninaamini hii benki inakwenda kufanya vizuri sana, kama mkiangalia katika benki zilizoko nchini, Mwalimu Commercial benki ndiyo benki ya wazalendo halisi.

"Benki hii ndiyo yenye wanahisa wengi zaidi kuliko benki nyingine yoyote ile, ina wanahisa 217,000, ni idadi kubwa kuzidi benki zote zilizo kwenye orodha ya soko la hisa la Dar es Salaam."





Mkulima wa zao la zabibu, Frida Josia, akivuna zao hilo katika Kijiji cha Matumbulu nje kidogo ya Jiji la Dodoma juzi. Kilo moja ya zabibu shambani inauzwa kwa bei ya 1,500/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jafo aeleza kukerwa ucheleweshaji hati

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameelezea kukerwa na kucheleweshwa kwa hati kwa ajili ya kuanza ujenzi wa tawi la Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, mjini Dodoma.

Hivi karibuni, Jafo aliagiza Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma kukabidhi hati ya eneo ambalo ofisi zao ziliungua, baada ya kukabidhiwa majengo ya TAMISEMI ili chuo hicho kijenge tawi lake ambalo kwa sasa liko kwenye jengo la kupanga linalogharimu Sh. milioni 75 kila mwaka.

Akizindua jana madarasa na nyumba za walimu wa chuo hicho kilichoko nje ya mji wa Dodoma, Jafo alisema alitoa agizo hilo miezi miwili iliyopita lakini bado kuna watendaji wanafanya kazi kwa mazoea na kukwamisha ujenzi huo.

"Mliniomba kujengwa kwa 'Town Campus' kutokana na majengo mnayotumia mnakodi kwa fedha nyingi. Nilipokuwa nazindua jengo la ALAT (Jumuiya ya Tawala za Mitaa) nilitoa maelekezo nikijua serikali hii ni tofauti na zilizopita kwa utendaji kazi. Nilitoa maelekezo kwa sababu ofisi zetu tulizokuwa tunakaa pale Mkapa House (ofisi ya TAMISEMI), Rais (John Magufuli) aliagiza jengo lile tukabidhi kwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

"Ofisi ya Mkoa ilikuwa na jengo lake ambalo liliwaka moto na kubaki kiwanja tupu, nikasema kwa kuwa mkoa unakuja kwenye ofisi ya TAMISEMI, kiwanja kile kimekaa miaka yote na kuna watumishi wa umma wapo mjini wanataka kusoma masomo ya jioni, ndiyo maana nikaagiza chuo cha Hombolo wapewe kujenga tawi lao," alisema.

Jafo alisema chuo hicho kimeshajipanga na kimetafuta fedha za kujenga majengo yake lakini bado kinakwamishwa kwa kutopewa hati.

"Watendaji bado wanazuga zuga, wanaturudisha kule kwa wahenga tulikotoka. Kuna watu wanajisahau, ndiyo maana nasema watu waliopewa madaraka wafanye kazi zao bila mazoea. Hadi leo hati ya kiwanja bado, Hombolo inaenda kujenga majengo ya serikali kuna shida gani, watu wengine ni wa ajabu," alisema. Waziri huyo alisema kuna watu ni wazembe na atalishughulikia ili ipatikane hati hiyo.

Akizungumzia ujenzi wa majengo hayo, Waziri Jafo alipongeza uongozi wa chuo kwa kutumia mfumo wa 'force account' ambao umesaidia kujengwa majengo manne kwa Sh. milioni 747 badala ya Sh. bilioni 1.5.

"Hii ni nusu gharama mliyokadiria, nawapongeza sana kwa kujenga majengo haya, nyie ni chuo cha mfano Tanzania kinachopaswa kuigwa, majengo haya mmejenga sio kwa fedha kutoka serikali kuu bali fedha za ada ya wanafunzi, mmewajengea miundombinu," alisema.

Mkuu wa Chuo hicho, Dk.Mpamila Madale, alimwomba Waziri Jafo kusaidia kupatikana kwa hati hiyo ili kuanza ujenzi kwa kuwa fedha tayari ipo.

"Imekuwa ikitugharimu Sh. milioni 75 kila mwaka kulipia pango kampasi ya mjini na mwaka huu tumeletewa hati ya malipo kodi imepanda itakuwa Sh. milioni 85, tuliona tujenge majengo yetu ili kuokoa fedha hizi nyingi tunazolipa," alisema.

Aidha, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21, chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 17,000 wakiwamo wa shahada ya utawala na menejimenti ya serikali za mitaa katika kampasi zote mbili na kujenga majengo mbalimbali.

## RC aunda kamati kuchunguza madai ya wafanyabiashara

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameunda kamati ya kutatua kero zinazowakabili wafanyabiashara wa soko jipya la Ndugai itakayofanya kazi kwa siku saba.

Hatua hiyo imetokana na wafanyabiashara hao kutoa malalamiko yao wakidai kuwa kuna watu wanapewa maeneo mara mbili au tatu.

Aidha, walisema biashara zao ni za duka lakini wamepewa vizimba jambo ambalo linahatarisha biashara zao huku wengine wakiwa na maeneo zaidi ya hayo.

Akizungumzia malalamiko hayo, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema uongozi wa jiji utachukua orodha ya wafanyabiashara ambao wanafanya biashara zao kwenye mazingira yasiyo rafiki ya soko hilo.

"Ni wale tu waliokuwa ndani ya viwanja vya Nanenane tutachukua orodha yao na suala zima ya wao kupata eneo tutalifanyia kazi kwenye baraza letu," alisema.

Kutokana na maelezo hayo, Dk. Mahenge alisema kamati hiyo inaundwa na watendaji kutoka Halmashauri ya Jiji na watu wa usalama ili kusiwe na udanganyifu.

"Ninawaomba muwe na utulivu tutashughulikia hasa watu waliodanganya na kuwa na eneo zaidi ya moja," alisema.

# Chuo kikuu chazindua jarida la Mnyampala

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Mtakatifu Yohana (SJUIT) cha jijini hapa, kimezindua jarida la Kiswahili la Mnyampala, huku kikiahidi kuendelea kuenzi kazi nzuri iliyofanywa na mtunzi wa kazi za fasihi nchini, Mathias Mnyampala.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jarida hilo jana jijini hapa, Mhariri wa Jarida hilo, Dk. Shadidu Ndossa, alisema chuo kikuu hicho kitaendelea kuzienzi kwa vitendo kazi zilizofanywa na Mnyampala ambaye ni marehemu.

"Ndio maana tumeanzisha jarida ambalo litatumia jina lake ambalo litakuwa likitoka mara moja kwa mwaka" alisema.

Dk. Ndossa ambaye anatoka Idara ya Kiswahili ya Chuo hicho, alisema pamoja na Mnyampala kuandika vitabu vingi, mchango wake bado haujatambulika, hivyo juhudi kubwa zinahitajika.

"Ni wazi kuwa wako wengi wanajiuliza Mathias Mnyampala ni nani. Ni mwandishi mahiri kutoka Mkoa wa Dodoma, hadi mauti kumfika aliandika vitabu vingi ambavyo vimeenea na kutapakaa kama Diwani ya Mnyampala, Maisha ni Kugharamia, Mashairi ya Hekima na Historia ya Kiswahili. Pia amewahi kuiandika historia ya rafiki yake mkubwa, Sheikh Aluta Amri Abeid," alisema.

Kuhusu jarida hilo, Dk. Ndossa alisema mchakato wa uanzishwaji wake ulianza mwaka 2017 na kwamba lina makala kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Zanzibar na Marekani.

"Mchakato huo ulienda sambamba na uteuzi wa bodi mbili za ushauri na uhariri baadaye mchakato ulikamilishwa kwa jarida kusajiliwa katika Makataba Kuu ya Taifa na kupatiwa namba za usajili.

"Tumeanzisha mchakato wa kulisajili jarida hili katika majukwaa ya kimataifa na Umataifa wa Jukwaa hili upo katika lugha ya Kiswahili,"alisema.


Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Taaluma) ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi huo, Prof. Timoth Simalenga, alisema jarida kama hilo ni la pili chuoni hapo na kwamba la kwanza lilihusu mambo ya sayansi.

"Hii ni siku ya kihistoria kwetu nikupongeze Ndossi kwa kuanzisha jarida hili pamoja na Idara ya Kiswahili hapa chuoni kwetu. Kuanza mapenzi ni raha, shida je, utaendeleaje? Hapo ndipo kwenye mchakato, sitarajii jarida hili liishie njiani," alisema Prof. Simalenga.

Alisema ni aibu watu kutoka nje kuja nchini kuandika historia na kufanya utafiti wa Mathias Mnyampala wakati wazawa wakiwa wapo.

"Watanzania sasa tufanye utafiti kuhusiana na Mathias Mnyampala. Wageni wanakuja wanafanya utafiti na sisi tufanye kwani ni aibu. Niwasihi kitumieni Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana kwani tutakuja na kitu kitaitwa St John Press," alisema.

Naye mwandishi wa vitabu mkongwe nchini na Mwenyekiti wa Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania (UKUTA) Tawi la Dodoma, Charles Mloka alikipongeza chuo hicho kwa kuanzisha jarida hilo. Alisema huo ni mwanzo mzuri wa kuzitangaza kazi za wabobezi wa Kiswahili.





# Shein ataka hospitali magonjwa mlipuko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema ni wakati wa Zanzibar kuwa na hospitali maalum ya kutibu maradhi ya kuambukiza ili kuwa katika nafasi nzuri ya kukabiliana na magonjwa yatakayojitokeza.

Dk. Shein alisema hayo jana Ikulu Zanzibar alipokutana na uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, ilipowasilisha taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi kwa kipindi cha 2019/20 na mpango kazi wa 2020/21.

Alisema ni jukumu la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuiamuru Wizara ya Afya kuchukua hatua za maandalizi ya ujenzi wa hospitali hiyo ikiwa ni hatua ya kujiweka tayari kukabiliana na maambukizi ya ugonjwa wowote utakaojitokeza, kama ilivyokuwa kwa maradhi ya corona, yalioibuka mwanzoni mwa mwaka huu.

Aliitaka Ofisi hiyo kuchukua hatua ya kukifanyia matengenezo kituo cha upataji nafuu na marekebisho ya tabia kilichoko Kidimni Wilaya Kati Unguja, ambacho kilitumika kuhifadhi wagonjwa waliokumbwa na maradhi corona baada ya maradhi hayo kusita tangu Juni, mwaka huu.

Pia aliagiza baada ya matengenezo hayo kukamilika, kukikabidhi kituo hicho Idara ya Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia ili kiendelee kutumika kwa shughuli zilizolengwa tangu kuanzishwa kwake.

Dk. Shein alitaka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kutoa msukumo wa kuhakikisha Ofisi ya Uratibu wa Mambo ya Muungano iliyoko Dar es Salaam inahamia Dodoma, kwa kuzingatia kuwa ndiyo makao makuu ya nchi, huku wizara zote za serikali ya muungano zikiwa tayari zimefanikisha jambo hilo.

Katika hatua nyingine, aliwataka viongozi, watendaji na wafanyakazi wa ofisi hiyo kufanya kazi kwa juhudi kubwa na kujenga misingi bora ya utumishi sambamba na kuepuka uvujishaji wa siri za serikali kwa kuzingatia kuwa serikali ina taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Dk. Shein alisema ana matumaini makubwa kuwa mgombea urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Hussein Ali Mwinyi, atashinda katika uchaguzi mkuu ujao kutokana na uwezo na sifa alizonazo.

Naye Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, aliwapongeza viongozi na watendaji wote alioshirikiana nao katika kipindi cha uongozi wa Dk. Shein na kuahidi kuendelea kumsaidia kiongozi huyo katika kipindi kilichobakia.

Aliwataka watendaji na wafanyaakazi kuendelea kupendana na kushirikiana sambamba na kuepuka chuki kwa kigezo kuwa hazina mchango wowote katika ujenzi wa Taifa.

Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, alisema katika kipindi hicho ofisi ilitekeleza kazi mbalimbali kwa mafanikio makubwa ikiwa pamoja na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kuratibu mapambano dhidi ya corona.

Alisema uratibu huo uliendana na utoaji wa elimu juu ya kujikinga na virusi vinavyosababisha maradhi hayo, ambapo jumla ya vikao 31 vya Kamisheni na Kamati ya Kamisheni vilifanyika.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji Zanzibar, Mustafa Aboud Jumbe (kulia), akisoma taarifa ya mpango kazi wa wizara hiyo kwa mwaka 2020/2021, katika kikao kilichofanyika Ikulu Mjini Zanzibar juzi, chini ya Mwenyekiti wake, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (hayupo pichani). Kulia kwake ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi. **PICHA: IKULU**

# Mufti asisitiza amani katika uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MUFTI wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabih, amesema ofisi yake itaendelea kuchukua juhudi za kuhakikisha Zanzibar na Tanzania kwa ujumla inaendelea kuwa na amani katika kipindi chote cha uchaguzi mkuu.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na watendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere waliofika katika ofisi hizo kwa ajili ya kuzungumzia amani katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Sheikh Saleh alisema tayari ofisi yake imeshaandaa utaratibu kupitia kamati ya amani kupita sehemu mbalimbali vikiwamo vyama vya siasa, masheha na watu wengine kwa lengo la kutoa elimu ya kulinda amani ya nchi.

Aidha, alisema amani na utulivu katika Tanzania ni tunu waliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu na kila mmoja anaihitaji katika masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

"Wananchi wanaihitaji amani, viongozi wanahitaji amani, wakulima wanahitaji amani ili kuendeleza kilimo chao mashambani, hivyo tuna kila sababu kwa gharama yoyote kuona tunaendelea kutunza amani ya nchi yetu," alisema.

Mufti alibainisha kuwa ziko nchi ambazo zimepoteza amani zikiwamo Libya, Iraq, Congo na Sudani na wanahitaji kuirudisha lakini wanashindwa.

Alisema kila mwananchi ana jukumu kubwa la kutunza amani ya nchi iliyopo katika mustakabali wa uchaguzi na kutambua kuwa kuna maisha baada ya uchaguzi.

"Lengo letu ni kuona amani ya nchi yetu inaendelea kama ilivyo sasa. Wananchi wanaendelea na shughuli zao za kujiletea maendeleo na tunataka katika kipindi chote cha ushaguzi, amani yetu inabaki kama ilivyo kwani amani ndiyo dira ya Watanzania," alisema.

Alisema ni matumaini yake uchaguzi utafanyika kwa salama na amani na kuundwa serikali ambayo itasimamia haki, usawa, amani na utulivu kwa Watanzania.

Aliiomba taasisi hiyo na Watanzania kwa ujumla kuendelea kushirikiana na kuwa kitu kimoja kuhakikisha wanaendelea kutunza amani iliyopo nchini.

Mkuu wa Fatwa na Utafiti wa Ofisi hiyo, Sheikh Thabit Noman Jongo, alisema wataendelea kuwatumia maimamu wa misikiti na maaskofu kuona wanahubiri amani katika kipindi chote cha uchaguzi na baada ya uchaguzi.

"Hatutaki kurudi nyuma tulipotoka kuwa na vurugu kama zilizotokea huko nyuma kila mmoja wetu anajukumu la kutunza amani kwa maslahi ya taifa na vizazi ya sasa na baadae," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere, Joseph Butiku, aliipongeza ofisi ya Mufti kutumia mbinu katika uchaguzi wa mwaka 2015 iliyofanikisha Tanzania kuendelea kuwa na amani na utulivu kwani imani na ibada.

## Wapewa elimu kuripoti kesi za udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MTANDAO wa kupinga udhalilishaji wilaya ya mkoani Pemba, umetoa elimu ya kuripoti kesi za udhalilishaji na kutoa ushahidi mahakamani kwa zaidi ya wanajamii 2,060 katika shehia 22 kuanzia Mei, mwaka huu.

Wajumbe wa mtandao huo walisema hayo wakati wa kikao cha uwasilishaji ripoti ya ufuatiliaji wa vitendo vya udhalilishaji katika ofisi za Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA).

Shaaban Juma Kassim Kutoka Jumuiya ya Wasaidizi wa Sheria Wilaya ya Mkoani, alisema katika kipindi hicho wajumbe wa kamati hizo waliandaa mikutano ya utoaji wa elimu katika makundi mbalimbali ya jamii zikiwamo shule, misikitini kwenye shehia pamoja na urushaji wa vipindi kupitia redio za kijamii.

Pia alisema kupitia utoaji wa elimu katika jamii juu ya athari za udhalilishaji na ushajihishaji wa jamii kuripoti kesi hizo zinapotokea, hatua hiyo imeanza kuleta mabadiliko katika jamii.

Alisema kutokana na juhudi hizo za kutoa elimu kwa wanafunzi, wameanza kuelewa athari za udhalilishaji na namna ya kuripoti kesi hizo. "Baada ya kuchukua juhudi hizi za kwenda kutoa elimu shuleni, tunashukuru hivi sasa wanafunzi wameanza kuelewa kuelewa udhalilishaji na matukio yamepungua kwa baadhi ya shehia," alisema.

Naye Abdalla Saleh Issa kutoka Jumuiya ya maendeleo ya Vijana (YACDES), alisema kupitia utoaji wa elimu ya stadi za maisha kwenye jamii wamewaunganisha vijana 15 kujishughulisha katika shughuli za ujasiriamali.

Mratibu wa TAMWA Zanzibar Ofisi ya Pemba, Fat-hiya Mussa Said, aliwataka wanamtandao huo kuongeza juhudi katika kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha vitendo hivyo vinatokomezwa.



**BURNA BOY SIASA ZITAKUPONZA** Uk.14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## DONGO TOSHA

# Harmonize ajigeuza tembo wanaomtukana vichwa chini

MWANAMUZIKI mkali wa BongoFleva, Harmonize, ameitambulisha ngoma yake mpya inayoitwa 'Jeshi' ambayo tayari imeibua mjadala mkali kutokana na maneno yake.

Tangu kuachiwa kwa ngoma hiyo wiki moja sasa, baadhi ya mashabiki wake wanasema ni dongo tosha kuelekea kwa mabosi wake wa zamani.

Ndani ya wimbo huo, Harmonize ameimba kwa kujisifu na kujitamba kwamba kutokana na magumu aliyopitia hatimaye amepata ushindi.

Harmonize ambaye awali alikuwa katika lebo ya WCB, aliamua kujiondoa na kuanzisha yake mwenyewe na kuita Konde Gang na kumletea mafanikio makubwa.

Baadhi ya mashabiki wake wamesema ngoma hiyo ni dongo lingine kwenda kwa washindani wake na kwamba ameonyesha jinsi anavyoweza kujisimamia.

Hata hivyo, amewasuta wale waliotamani kuona anaanguka baada ya kuwa peke yake, kwa kuwaambia sehemu ya mashairi yake "Wale walionitukana vichwa vyao vipo kibra, siku hizi siimbi sana wanashindana na Ibwarh."

Kisha akajisifu kwa kujifananisha na Tembo ambaye anapotembea mbugani hana adui dhidi ya wanyama wingine, na kama binadamu basi sawa na jeshi kutokana na kuhimili mapigano.

BASI SAWA

## He! Mzee Yusuph hanaga ndevu za sineri

MFALME wa Muziki wa taarab, Mzee Yusuph, ambaye amerudi tena jukwaani baada ya kukaa nje kwa muda wa miaka saba, ametupa dongo hewani baada ya kusema wanaodhani kwamba amekwisha basi wamepotea.



Akizungumza na EATV, Mzee Yusuph, amesema mashabiki bado wana hamu naye na walikosa burudani yake kwa muda mrefu, hivyo kurudi kwake kumewapa furaha kwa sababu yeye sio mzee mwenye ndevu za sineri.

"Watu walisema hawataki muziki kumbe wanataka sana, kwa hiyo bado wanahaja na wanahitaji, pengo langu halijazibika na nafasi yangu ilikuwa kubwa sana kwenye huu muziki na hicho ndicho kilikuwa kimekosekana na kupotea lakini sasa kimerudi, hakuna kiapo cha maskini, kauli yangu ipo na itaendelea kuishi, uamuzi wangu ni sahihi, mimi sio mtu mzima na sina ndevu za sineri" amesema Mzee Yusuph.

## Shetta leba ulifuata nini?

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Shetta, amefunguka kwa kueleza ameshuhudia ushujaa wa mwanamke pale alipobahatika kuingia leba kushuhudia mtoto wake wa pili akizaliwa.



Amesema akiwa katika chumba hicho, alishuhudia tabu alizopitia mkewe mama Qaylah na hapo aliamini hakuna mwanamke mdhaifu, bali wana ujasiri wa hali ya juu.

Shetta amesema wanawake ni watu ambao wanatakiwa kuheshimiwa sana kwa sababu ya kitendo cha kulea.

"Nilimuona mke wangu Mama Qaylah wakati yupo leba anajifungua mtoto wetu wa pili, nafikiri wanawake ni watu ambao tunatakiwa tuwaheshimu sana, kwa sababu kitendo cha kubeba ujauzito miezi 9, ile hali ya kujifungua inakuaga ni nusu kifo na kazi kubwa " ameeleza Shetta.



## Mr Blue akumbuka ukiwa

RAPA mkongwe ambaye bado anafanya vizuri, Mr Blue, amekumbuka jinsi alivyochanganyikiwa kutokana na kupitia magumu baada ya kifo cha mama yake.

Mr Blue amesema sasa hivi anajiona mpweke kama nyani mzee, kwa sababu mama yake na ndugu zake wengi wametangulia mbele yaki akiwamo baba yake.

Hata hivyo, msanii huyo amesema mtu pekee anayemfariji ni mkewe Wahda, akisema anampenda sana kwa sababu amemvumilia mengi.

## Tatu Katatuta Dunia kigeugeu

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote dunia haitabiriki. Leo unaweza kuwa hivi kesho vile. Unaweza ukawa meneja, kesho ukatimuliwa ukaishia kuhangaika na njia.

Kuna mwanamuziki mmoja mwanamama kutoka Congo DR anaitwa Lady Issa, aliimba wimbo mmoja unaoitwa 'Dunia', ambao baadhi ya maneno yake yanaelezea jinsi maisha yanavyogeuka.

Hebu ipitie filamu hii inaitwa 'Katakuta' ambayo inaweza kukuweka wazi na kuelewa binadamu walivyo na jinsi dunia inavyowaumbua.

Walioigiza ni Medebe Lidai, Muhogo Mchungu, na wengineo wengi. Inaanza kwa kuonyesha kuwa Muhogo Mchungu anaishi na mkewe, pamoja na binti yao Tatu. Maisha yao hayakuwa mazuri. Mke wa Muhogo Mchungu yeye maisha yake alikuwa anamkuwadia binti yake Tatu kwa wanaume.

Tatu ni binti aliyeumbika hasa, lakini tabia yake haikuwa nzuri. Nyumbani hapo wana mpangaji wao wa kike Zubeda.

Yeye alikuwa mpangaji mwenye heshima na nidhamu, kiasi kwamba hata kama Tatu na mama yake wakikosa kumpikia chakula Muhogo Mchungu, basi yeye atampelekea.

Vitendo cha Tatu na mama yake vilikuwa havimpendezi kabisa mzee huyo.

Kwenye nyumba hiyo anakuja kupanga mpangaji mmoja Bonge Mzito. Ni mfanyabiashara wa chips. Tatu na mama yake wanachukua fursa hiyo kumchuna. Mipango inafanywa ili Tatu ajipitishepitishe kwa Bonge. Mipango inafanikiwa. Bonge na Tatu sasa wanakuwa wapenzi. Tatu na mama yake sasa hata kupika hawapiki, ni mwendo wa chips kwa kwenda mbele.

Mbaya zaidi, Tatu na mama yake wakafanya mpango ili ajifanye ana mimba, wapate kutumia pesa zake vizuri.

Bonge anashtuliwa na baadhi ya majirani kuwa mpenzi wake hana mimba, ila anaigiza tu.

Anaamua kumpeleka mpenzi wake hospitali ili akahakikishe. Mchezo unachezwa, mama mtu anamfuta mama mjamzito na kumhonga pesa, akachukua haja ndogo yake ikapelekwa hospitali kwa madai kuwa ile ndiyo ya Tatu. Hospitali wanathibitisha kuwa Tatu ni mjamzito baada ya kuletewa sampo ya haja ndogo.

Siku zinakwenda hakuna dalili yoyote si ya kujifungua tu, bali hata mimba kukua.

Bonge Mtata, alianza kuchoka na mambo ya Tatu na mama yake. Akakumbuka maneno ya wenzake kuwa wanachofanya ni kumlia pesa zake na kumfilisi biashara yake.

Hatimaye anagudua kuwa alikuwa anadanganywa, hivyo anavunja uhusiano wa kimapenzi na Tatu.

Bonge anaanzisha uhusiano na Zubeda na kutaka kumuoa kabisa mpangaji ambaye alikuwa hapendwi na Tatu na mama yake, ila mzee Muhogo Mchungu tu.

Zubeda anapata ushauri kutoka kwa mzee Muhogo Mchungu, na majirani kuwa aolewe tu.

Harusi kubwa na ya kufana inafanyika kati ya Zubeda na Bonge Mtata.

Wote walifurahi, kasoro Tatu na mama yake ambao hawakuhudhuria harusi hiyo badala yake walikaa pembeni wakiwa wamenuna na kufura kwa hasira kama kobra aliyekanyagwa mkiani.





## Ebitoke unalitafuta domo la Gigy Money

MSANII wa vichekesho, Ebitoke, amefunguka kwa kusema anamchukia Gigy Money kutokana na tabia yake ya kuropoka ovyo.

Ebitoke amesema kamwe hawezi kumkubali Gigy Money kwani aliwahi kumsikia akimuongelea kwenye mahojiano jambo ambalo hakupendezwa nalo.

"Nikiongelea kuhusu Gigy Money na Nandy kwanza mimi simkubali Gigy halafu huwezi ukamfananisha na Nandy, yeye anaropoka kila kitu hawezi kuweka siri, nimewahi kumsikia anaropoka kuhusu mimi na 'ameniblock' tangu naanza kujulikana mwaka 2016, simuogopi na hata moto aliokuwa nao na mimi nauweza" amesema Ebitoke.






## Usinifokee, Ni yeye misemo 'iliyotrendi'

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA inaenda kasi sana. Leo unaweza kukuta watu wanafanya hivi, lakini kesho wakabadilika na kufanya vile. Ndiyo maana kwa sasa usikariri maisha.

Kila kukicha kila kitu kinabadilika. Hata misemo nayo inabadilika. Hapo nyuma kidogo kulikuwa na misemo kama 'mabaharia' na mingine mingi.

Hivi sasa kuna misemo mingine kabisa. Ingawa ukiisikiliza si mipya, lakini sababu kubwa ya 'kutrendi' ni kusemwa au kutolewa na watu maarufu kama vile wanamuziki, wasanii, wanamichezo, waigizaji na watu wengine ambao wanaushawishi kwenye jamii.

Leo tunawaletea misemo kadhaa ambayo 'ilitrendi' huko nyuma na hii ya sasa, pamoja na watu maarufu walioitambulisha au kuitunga misemo hiyo.

**MI' NA MABINTI DAMU DAMU-MWANA FA**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, msanii wa muziki kizazi kipya, Mwana FA, alitoa ngoma aliyoiita 'Mi na Mabinti Damu Damu.' Ni ngoma iliyopendwa na kutoa msemo huo hasa kwa vijana ambao wanaonekana kuwa hawajatulia, wenye kupenda mademu wengi wakaitwa 'wao na mabinti damudamu.'

**HABARI NDIYO HIYO-MWANA FA**

Naweza kusema kuwa hapa Tanzania hakuna msanii ambaye ametengeneza misemo mingi 'iliyotrendi' kama Mwana FA. Huyu unaweza kumwita ni baba wa misemo ya Kibongo.

Alitoa ngoma iitwayo 'Habari Ndiyo Hiyo'. Jina la ngoma hii nalo likawa msemo 'uliotrendi' sana Bongo. Mtu alimwambia mtu kitu akashangaa, au akimpasha ukweli atamwambia 'habari ndiyo hiyo.'

**UNANITEGA?- MWANA FA**

Ilikuwa ni katikati ya miaka ya 2000, Mwana FA kama kawaida yake akatoa ngoma nyingine akaiita 'Unanitega?' 'Mbona miguu iko wazi unanitega? (aa-aaa), kifua kiko wazi unanipenda? (hebu huko).

Msemo huu nao ulitawala sana hasa kwa vijana kwenda kwa wasichana ambao walionekana kuvaa nguo zisizo na stara wanapopita mbele yao.

**BADO NIPO NIPO KWANZA-MWANA FA**

Mwana FA bado anendelea kutamba hapa, kwani hakuishia hapo, alionyesha kuwa yeye ni mfalme wa misemo, akaja na ngoma ya 'Bado Nipo Nipo Kwanza' unaomzungumzia kijana ambaye bado hataki kuoa kutokana na dosari kadhaa anazoziona kwa baadhi ya wanandoa. Sasa ikawa kijana ambao hawajaoa wakaanza kuitwa majina hayo.

**INGEKUWA VIPI?-MWANA FA**

Unakumbuka ule msemo wa 'ingekuwa vipi?'. Hii ilitokana na ngoma ya Mwana FA alioiita 'Ingekuwa Vipi?'.

**AHSANTENI KWA KUJA-MWANA FA**

Msemo huu nao 'ulitrendi' miaka si mingi iliyopita kutokana na Mwana FA kutoa ngoma moja alioiita 'Ahsanteni Kwa Kuja'.

Unan'taka Kwio-Meja Kunta

Msanii wa Singeni, Meja Kunta, yeye alikuja na msemo ambao kwa sasa 'unatrendi' sana hasa kwa akinadada wa 'unamtaka kwio, unahela kwio, kwio hiyo kwio'. Hii ilitokana na ngoma yake ya 'Wanga'.

**USINIFOKEE-BABA LEVO**

Msanii Baba Levo naye hivi karibuni ametoa msemo wake ambao unatamba mitaani na kwenye mitandao wa kijamii usemao 'Usinifokee'.

**NI YEYE-TID**

Ni msanii mkongwe ambaye ni mwanzilishi wa msemo wa 'Ni Yeye'. Hivi karibuni ameonekana akilalamika kuwa amechukuliwa msemo wake na watu wanautumia bila yeye kupata chochote.

# Big Brother Nigeria 2020 yanoga



SHINDANO la Big Brother Nigeria 2020, limeanza rasmi na baadhi ya washiriki wanaonyesha kuwa moto mkali.

Lucy na Erica ni miongoni mwa washirki wanaowavutia watazamaji kutokana na vituko vyao. Wiki hii wakiwa wamekaa kwenye korido wakiwa na Ozo, walifanya umbea kwa kueleza mmoja wao anahitaji kuwa karibu kimapenzi na Kiddwaya.

Lucy ndiye aliyekuwa wa kwanza kusema anakuwa mbali na uhusiano wa kimapenzi ndani ya nyumba hiyo.



## Arnold waambie wanaolilia penzi

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Arnold Olatunde, amewakumbusha vijana kwamba ni rahisi kuanguka kimapenzi kama akili na matamanio hayatadhibitiwa.

Akizungumza katika kipindi cha Tv kinachozungumzia mapenzi, Mwigizaji huyo alisema kuanguka penzi ni rahisi kuliko kulijenga, hivyo inahitaji uwekezaji mkubwa wa kiakili kwa watu wanaopendana.

"Ni rahisi kuanguka kwa penzi kwa wakati huu wa sasa, lakini kubaki ni jambo lingine kwa sababu penzi ni suala la asili, hata mimi huu ni muda wa kujifunza," amesema.

## Prince Harry, Meghan wanunua hekalu lao

MWANAMFALME Harry na mkewe Meghan Markle, imeelezwa tayari wamenunua jumba la kifahari kwa ajili ya makazi yao mapya.

Kulingana na mtandao wa pageSix, jumba hilo la kifahari lipo eneo la Montecito, California Marekani.

Taarifa hizo zinaeleza nyumba hiyo ina kila kitu ndani ikiwamo vyumba 16 vya kulala, bustani iliyopambwa kwa maua na miti ya mizaituni, uwanja wa tenis, mgahawa maalum, chumba cha michezo kwa watoto na bwawa la kuogolea.





## Favour kumbe kidume bhana!

MWANAMUZIKI mkali wa Nigeria, Chinedu Okoli, maarufu kama Flavour, imeelezwa anaongoza kwa kujihusisha kimapenzi na wanawake warembo.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa, umebaini kwamba, Flavour ambaye hivi karibuni ameripotiwa kufunga ndoa na mpenzi wake wa zamani, alikuwa na uwezo wa kuchagua warembo.


Baadhi ya warembo hao aliotoka nao kimapenzi ni Beverly Ukegbu, Anna Banner, Sandra Okagbue, Juliet Oluchi Ehiemere, Chidinma Ekile na Onyinye Onungwa.

## Burna Boy siasa zitakuponza

STAA wa muziki wa Afro-pop, Burna Boy, ameibua mjadala mkali baada ya kueleza anachokiamini kuhusu wazo la Afrika kuwa moja kimtazamo.

Akizungumzia mtazamo wake, Burna Boy, amesema yeye ni mfuasi mkubwa wa aliyekuwa kiongozi wa Libya, Muammar Gaddafi, ambaye aliamini kuungana kwa nchi za Kiafrika ndio njia pekee ya kujikomboa na ubeberu,

"Yote ni ujinga, Muammar Gaddafi, amesema umoja wetu ni ukombozi wetu, mimi naamini hivyo kwa sababu ni njia bora na inaweza kutusukuma kwenye uso wetu," amesema



MAKALA

# Corona inavyoacha somo kinamama kujikinga na magonjwa ya milipuko

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI serikali imetangaza kupungua kwa maambukizi ya virusi vya Corona, bado wananchi wanahimizwa kuendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kujikinga na ugonjwa huo.

Baadhi ya hatua zinazopendekezwa ni kunawa mikono kila mara, kujisafisha kwa kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kujiepusha na mikusanyiko isiyo ya lazima.

Valentina Kasian (45), mkazi wa Tabata, jijini Dar es salaam, ambaye ni mchuuzi wa matunda eneo la Tabata kwa Sesi, ni miongoni mwa watu wanaokiri kujisahau kujikinga dhidi ya virusi vya corona.

Akizungumza na mwandishi wa makala hii, Valentina ambaye hutumia saa 12 akiwa kwenye shughuli zake za biashara, amesema kwa sasa tahadhari kwake si jambo la muhimu kwa kuwa ugonjwa umekwisha .



Wanawake wakiendelea na biasahara zao katika moja ya masoko nchini. **PICHA: MTANDAO**

Kutokana na biashara yake ambayo inambidi kutembea mitaani, hatari ya kuambukizwa inakuwa kubwa.

"Natumia kama masaa matatu hivi, kuzungukia nyumba zote za maeneo haya ya kwa sesi kuuza mtunda, kisha narudi nyumbani kuhudumia familia", anasema.

Mama huyo mwenye watoto wawili anakiri kuwa umakini wa kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona kwenye baadhi ya maeneo kama ndani ya daladala na sokoni umepungua.

Anasema imefikia wakati utaona mtu mmoja au watu wawili pekee ndio wanaonekana kuvaa barakoa, jambo ambalo ni hatari.

"Sokoni nako ni hivyo hivyo, ile taharuki ya ugonjwa imepotea kabisa, soko zima unaweza kuona mtu mmoja ndio amevaa barakoa, hata mimi pia sizingatii kwa kweli".anasema

Mama huyu ni mmoja kati ya asilimia zaidi ya 80 ya wanawake wanaotajwa na Shirika la kazi Duniani (ILO) katika utafiti wa mwaka 2006 ambao wanafanya kazi zao katika maeneo yenye mikusanyiko ya watu.

Kutokana na takwimu hiyo, wanawake hao wanaonekana kuwa hatarini kupata maambukizi ya ugonjwa wa Corona na kuathiri shughuli zao za kiuchumi.

Amina Ramadhani, mfanyabiashara wa mbogamboga anayetembeza mtaani, anakiri kuwa ana muda mrefu hajafuata tahadhari ya kujikinga virusi vya corona.

Anaeleza kwamba hana haja ya kuvaa barakoa anapokuwa katika shughuli zake kwa sasa kwa kuwa dalili zinaonyesha umepungua.

"Kwa kweli sijazingatia, hata unavyoniona hapa sina hata barakoa ingawa kwa wakati mwingine naogopa kama ugonjwa huu ukirudi tena naweza kuambukiza hata watoto nyumbani na kushindwa kufanya shughuli zangu ," anasema Amina

Amina anatamani uhamasishaji urudi kama ilivyokuwa mwanzo ili watu waendelee kujikinga.

Vilevile vitendo vya kutokuwa makini kwa kuzingatia maagizo yanayotolewa kwa baadhi ya wanawake, inaelezwa kuwa ni moja kati ya vitu vinavyoweka hatari ya kusambaa kwa kasi kwa corona.

"Sisi wanawake hatuuzingatii kabisa, unajua ni mtu wa kwenda kwenye mikusanyiko ya watu, kwa nini usichukue tahadhari" anaongeza kusema.

Kisha anaendelea "Mimi ni mama wa familia, ninapoambukizwa ugonjwa huu inamaana nitaambukiza familia yangu yote nyumbani kwa kuwa dalili zake hazijitokezi hapo hapo unapoambukizwa," anasema

Kwa upande wa Bertha Philimon, mmiliki wa duka la nguo Kariakoo, anasisitiza wanawake kuendelea kuchukua tahadhari kwa sababu wao ndio walezi wa familia.

'Kwa mfano mimi mtu haingii dukani kwangu bila ya kuvaa barakoa na kunawa mikono, kwa sababu ugonjwa huu upo, tunapaswa tuishi nao kwa kuchukua tahadhari." Anasema Betha.

Kipato cha Betha katika duka lake ni kati ya Sh. 300,000 hadi 500,000 kwa siku kwa sasa, nusu ya mapato yamepungua tangu kutangazwa kwa ugonjwa wa corona.

## ATHARI UCHUMI

Mkurugenzi wa Taasisi ya Binti makini, Janeth Makini, anaelezea athari za Covid-19 kwa wanawake kuwa ni nyingi lakini kubwa ni kushuka kwa uchumi kutokana kudorora kwa biashara.

"Wanawake wajasiriamali wengi kwa sasa wamedhoofika kiuchumi, wengine wameshindwa kurudisha marejesho ya mikopo na hata kupeleka watoto shule, na kuna ambao wamelazimika kuuza vitu vyao vya ndani ili kusimamisha tena biashara zao ,"anasema Janeth.

Kwa mujibu wa mwanaharakati huyu, wakulima vijijini nao corona imewatafuna, akitolea mfano wa wakulima mkoani Lindi, ambao wamelazimika kuuza zao la korosho kwa Sh. 800 Badala ya bei elekezi ya Sh.3000 kutokana kukosa wateja.

## ELIMU YAENDELEZWA

FORUM CC ni Taasisi inayojishughulisha na kutoa elimu mbalimbali ikiwemo athari za Mabadiliko ya tabia nchi na wanawake(FORUMCC), kwa kushirikiana Umoja wa Ulaya (EU), inaendelea kuhamashisha wanawake kuendeleza tabia njema ilizojifunza kutokana na ugonjwa wa Covid-19.

"Tumeona ni vizuri kuendeleza tabia njema tulizojifunza kutokana na ugojwa wa corona kama vile kunawa mikono,kuvaa barakoa unapokwenda kwenye sehemu yenye mikusanyiko mikubwa ya watu na pia kutunza mazingira ili kuchukua tahadhari ya magonjwa yanayoambukiza kama corona" alisema Sara Pima, Ofisa Mradi wa ForumCC

## COVID-19 VS MAFUA YA HATARI

Akiongelewa tofauti ya ugonjwa na Covid-19 na homa ya kawaida, Dk. Neelum Ismail kutoka hospitali ya Agakhan, anasema kuwa magojwa haya hutokana na virusi tofauti.

Kwa mujibu wa Daktari huyo wa familia, Covid-19 hutokana na virusi vya corona na huambukiza kwa kasi kuliko kirusi cha mafua kiitwacho influenza.

Vilevile huathiri mfumo wa upumuaji wa mwanadamu na huweza kuibua maradhi mengine kama vile homa ya mapafu na figo kushindwa kufanya kazi.

## HALI ILIVYOKUWA

Mnamo Machi 16, 2020, Tanzania ilitangaza mgonjwa wake wa kwanza wa virusi vya Covid19 na Machi 17, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa alitangaza kufunga shule zote kuanzia za awali hadi vyuo vikuu.

Pia serikali ilizuia mikusanyiko yote na kuzuia safari za kimataifa zisizo na ulazima ili kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa Covid -19 nchini.

Pia alitangaza kutolewa Sh. milioni 500 kati ya Sh. bilioni moja zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Mbio za Mwenge wa Uhuru ili zisaidie katika kukabiliana na janga hili.

## HATUA KUDHIBITI COVID-19

Jitihada zilizofanywa na Rais John Magufuli, zilisababisha kuwepo na umakini katika kutoa elimu kwa umma kuhusu mlipuko wa ugonjwa wa corona, dalili zake pamoja na jinsi ya kuepuka maambukizi.

Jamii ilielimishwa umuhimu wa kunawa mikono kwa maji tiririka mara kwa mara,kutumia vitakasa mikono, kuvaa barakoa na kuepuka msongamano kwa kuzingatia umbali baina ya mtu mmoja na mwingine.


## MITISHAMBA KUTUMIKA

Katika harakati za kujikinga na ugonjwa corona kulienea imani kuwa mchanganyiko wa baadhi ya mitishamba 'nyungu' kuwa na uwezo wa kuua vimelea vya ugonjwa wa corona pale mtu anapojifukiza.

Moja na dawa zilizouzwa ni NIMRCAF iliyotengenezwa na Taasisi ya Taifa ya utafiti wa magonjwa ya binadamu-NIMR.

## SHUGHULI KUFUNGULIWA

Mwezi Mei mwaka huu, Serikali ilitangaza shughuli za kawaida za kijamii, kiuchumi ziendelee kama kawaida hali iliyopelekea kufunguliwa kwa shule za msingi, sekondari na vyuo.



MAKALA

# SHAKUNTALA DEVI

## ■Mwanamke anayehesabu kuliko kompyuta
## ■Atengenezewa filamu kama shujaa wa dunia

**Na Mwandishi wetu**

HAIJAWAHI kutokea! Ndivyo wasomi wengi duniani wanavyomuongelea Shakuntala Devi, mwanamke ambaye anatajwa kuwa ni kiumbe mwenye uwezo mkubwa wa kufanya hesabu kwa kutumia ubongo wake kuliko binadamu yoyote.

Shakuntala ambaye sasa ni marehemu alikuwa na uwezo wa kufanya hesabu sekunde kadhaa hali iliowafanya watu kumuita jina la 'Kompyuta'.

Kipaji chake cha ajabu kilimfanya kushinda tuzo ya Guiness katika nafasi ya rekodi ya dunia kama mtu maarufu aliesafiri duniani kutoa majibu ya hesabu.

Kutokana na umaarufu wake, mwanamke huyo mzaliwa wa India, alipata mialiko mbalimbali vyuo vikuu maarufu duniani, kumbi za filamu, vituo vya radio na runinga.

Mwanamke huyu aliefariki mwaka 2013 akiwa na umri wa miaka 83.

Katika kumuenzi kumetengenezwa filamu ya maisha yake iliyotolewa hivi karibuni katika ukumbi wa Amazon.

Mwigizaji wa filamu kutoka Hollywood, Vidya Balan, alimtaja kama msichana kutoka mji mdogo wa India aliyeushangaza ulimwengu.

"Hakuwa na elimu, lakini alikuwa na kipaji cha kutatua hesabu ngumu zaidi kwa kutumia ubongo wake kwa kasi ya kushangaza. Alikuwa na kasi kama ya kompyuta",Balan ameiambia BBC.

Mwigizaji huyo alijifunza masuala mengi kupitia kanda ya video kutoka Canada ambayo inamuonyesha Devi akiliuliza jopo iwapo linataka kupatiwa majibu kuanzia kushoto kwenda kulia au kutoka kulia kwenda kushoto.



**Katika utafiti wa mwaka 1990, Authur R Jensen , mtafiti wa intelijensia ya binadamu katika chuo kikuu cha California ,USA, alimtaja mwana mama huyo kuwa mtu makini, anayetumia muda wake mwingi vizuri, mwenye tabia njema na mtu fasaha.**

Kanda hiyo ya video imesambazwa zaidi ya mara 500,000, tangu ilipochapishwa mwaka 2013.

**MIKONO YA MUNGU**

Katika mahojiano, Shakuntala anasema kwamba alifanya hesabu tangu alipokuwa na miaka mitatu.

Baba yake mzazi ambaye alikuwa mchezaji wa sarakasi, aligundua kipawa chake wakati walipokuwa wakicheza karata na kubaini kwamba binti yake alikuwa akimshinda kwa sababu alikuwa na uwezo wa kukariri karata zake.

'Ni zawadi kutoka kwa Mungu', alikuwa akisema alipoulizwa kuelezea kipaji chake cha ajabu.

Devi alifanya hesabu ngumu kichwani bila kuhitaji kuandika mahali popote.

"Hakuna hata mtu mmoja katika familia yao aliyekuwa na kipaji chochote cha mahesabu, licha ya kwamba baba yake alikuwa akifanya mazingaombwe", alikakaririwa akisema wakati mmoja.

Akiwa na umri wa miaka sita pekee, tayari alitambuliwa kama mtoto aliependa hesabu, alionyesha ujuzi wake kwa mara ya kwanza katika hafla moja katika mji wa Mysore, Karnataka.

**UWEZO WA KIPEKEE**

Mwaka 1950 , aliposhiriki kipindi cha televisheni cha BBC, alitoa jibu la hesabu ambayo haikuwa sawa na ile ya mwandalizi wake.

Hata hivyo, Shakuntala alifafanua kwamba kulitokana na makosa ya watu waliotoa.

Wataalamu walipochunguza tena nambari hiyo walikubaliana kuna makosa.

Katika jambo la kushangaza, mwaka 1977, mjini Dallas, Marekani , mwanamke huyo aliishinda kompyuta aina ya Univac, mojawapo ya kumpyuta zilizokuwa na kasi zaidi duniani.

Na katika shindano la kuingia katika vitabu vya dunia vya Guiness , alishinda kwa kuzidisha nambari mbili za nambari 13 zilizochaguliwa kutoka maeneo tofauti na kompyuta mbele ya umati wa watu 1000 katika chuo cha Imperial mjini London.

Alichukua sekunde 28 kukamilisha hesabu hiyo, ikiwemo muda aliochukua kusoma jibu la nambari 26.

**VIPAJI VINGINE**

Pamoja na ubongo wake kuwa na kasi kubwa kuhesabu, Shakunlata alikuwa na kipaji kingine cha kutabiri mambo mbalimbali.

Aliandika vitabu kuhusu unajimu, upishi, hesabu, na uhalifu.

"Yote haya yalinipatia wazo kuhusu maisha yake . Kile kilichonivutia mimi ni kwamba watu huhusisha mchekeshaji na hesabu na hubadilisha wazo hilo kabisa", anasema mwigizaji huyo ambaye amecheza kama Shakuntala.

"Alicheza na namba, uliweza kuona akifurahi ndani yake alipofanya hesabu", anaongeza.

Katika utafiti wa mwaka 1990, Authur R Jensen , mtafiti wa intelijensia ya binadamu katika chuo kikuu cha California ,USA, alimtaja mwana mama huyo kuwa mtu makini, anayetumia muda wake mwingi vizuri, mwenye tabia njema na mtu fasaha.

Hata hivyo, inaelezwa mpaka anafariki hakuwa na furaha kutokana na ukweli kwamba kipaji chake hakikuweza kumpatia fedha.

Katika mahojiano yake mengi , Shakuntala alielezea kwamba wakati akiwa mtoto, alikuwa chini ya shinikizo kupata fedha kwa ajili ya kusaidia familia yake.

"Nina shahada ya udaktari katika hesabu na sijui kugawanya na takwimu tatu au jinsi ya kuhesabu mraba kwa mkono". Alisikika akisema wakati mmoja.

Hata hivyo, Balan anatumai filamu hiyo itawaburudisha watu wengi.

Anatumaini filamu hiyo italeta mabadiliko jinsi watu wanavyofunza hesabu , kulifanya kuwa somo la kuvutia na kuondoa hofu ambayo watu wanayo.

**Kwa msaada wa mtandao.**

HABARI KIMATAIFA

# Pombe yazalishwa kisiri chuo kikuu

**LUSAKA, Zambia**

KATIKA hali ya kushangaza, chuo kikuu kimoja nchini Zambia, kimejikuta kikihaha kutafuta ufumbuzi baada ya kugundulika ndani ya majengo yake kuna kiwanda cha kutengeneza pombe.

Mamlaka katika mji mkuu wa Lusaka, umesema umebaini kuwapo kwa kiwanda cha mvinyo ndani ya chuo hicho ambacho kinaendeshwa kinyume na sheria.

Kulingana na mtandao wa Lusaka Times, maofisa wa afya walitoa taarifa baada ya kupokea malalamiko kutoka uongozi wa chuo cha Evelyn Hone, wakilalamika kuwapo kwa harufu mbaya iliyokuwa ikitokea upande wa mgahawa wa chuo..

Baada ya ufuatiliaji zaidi, maofisa hao waligundua kiwanda hicho ambacho kilikuwa na uwezo wa utengenezaji wa mvinyo pamoja na uzalishaji wa chupa zake.

Mmiliki wa kiwanda hicho, alijitetea kuwa alishindwa kupata kibali cha kutengeneza na kusambaza pombe hiyo hali iliyomlazimu kuendesha bila usajili.

Bado haijawekwa wazi iwapo mmiliki wa kiwanda hicho ndiye mmiliki wa mgahawa huo pia.

**BBC.**



Baadhi ya wanakijiji wa Karo wakiangalia volcano ikipaa angani baada ya kulipuka kutoka mlima wa Sinabung, Kaskazini mwa Sumatra nchini Indonesia juzi.**(PICH:AFP)**

# Ndege ya kijeshi Marekani yapigwa risasi

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la Ujasusi la Marekani, limeanzisha uchunguzi baada ya helikopta ya kijeshi karibu itunguliwe kwa risasi kwenye mazoezi ya kawaida katika jimbo la Virginia.

Katika tukio hilo lililotokea siku ya jumatatu, mtu mmoja alijeruhiwa na helikopta hiyo ikalazimika kutua kwa dharura.

Maofisa wanasema kwamba ndege hiyo ilikuwa inapaa umbali ya takriban futi 1,000 kutoka ardhini wakati ilipopigwa risasi.

Tukio hilo lilitokea majira ya mchana kilomita 16 kutoka uwanja wa ndege wa Manassas, kaskazini mwa Virginia.

Helikopta hiyo ilitua kwa dharura katika uwanja wa ndege baada ya kupigwa risasi.

Mfanyakazi wa ndege hiyo aliyejeruhiwa alipelekwa hospitali na aliruhusiwa kwenda nyumbani.

Taarifa kutoka Jeshi la Anga, ilisema kuwa ndege hiyo ya helikopta aina ya UH-IN Huey, imeharibika kiasi.

Helikopta hiyo inafanya kazi ya kusafirisha wanajeshi waandamizi, viongozi wa kiraia pamoja na wageni wengine waheshimiwa, na wagonjwa wakati wa dharura.

Shirika la Upelelezi la Marekani (FBI) limesema linashirikiana na mashirika mengine ikiwemo ofisi ya jeshi la angani inayoshughulika na uchunguzi maalum kutathmini kile kilichotokea.

Maofisa hao walisema risasi hiyo ilifyatuliwa na mtu aliyekuwa ardhini lakini bado haifahamiki ikiwa ndege hiyo ilipigwa risasi kimakusudi au ajali iliyosababishwa na ufyatukaji wa risasi.

**BBC.**

# Uturuki, Iran yalaani makubaliano ya Israel

**ANKARA, Uturuki**

NCHI za Iran na Uturuki zimeshutumu vikali makubaliano yaliyofikiwa kati ya Israel na Umoja wa Falme za Kiarabu kurejesha mahusiano yao ya kidiplomasia.

Makubaliano hayo pia yanahusu kusitishwa kwa mpango wa Israel, kunyakua eneo la Wapalestina katika eneo la Ukingo wa Mto Jordan.

Makubaliano hayo kati ya Israel na Umoja wa Falme za Kiarabu, ambayo yalitangazwa na Rais wa Marekani Donald Trump juzi Alhamis, ni ya tatu kufikiwa kati ya Israel na taifa la Kiarabu.

Katika makubaliano hayo, Israel imeahidi kusitisha unyakuaji wa ardhi ya Wapalestina, licha ya kuwa Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu anasisitiza kuwa haina maana ya kuacha kabisa mipango huo.

Mataifa hayo yalisema makubaliano hayo sawa na usaliti kwa mapambano ya Wapalestina.

**DW.**

# EU kuijadili Belarus, Uturuki

**BERLIN, Ujerumani**

MAWAZIRI wa mambo ya kigeni wa Umoja wa Ulaya (EU) wanajadili kuhusu uwezekano wa kuiwekea vikwazo nchi ya Belarus na eneo la mashariki mwa Bahari ya Mediterania.

Mkutano huo ambao unafanyika kwa njia ya video, utatoa dira ya hatua gani za haraka zichukuliwe.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, ameitisha mkutano huo maalum baada ya kukatiza mapumziko yake kutokana na mambo yanayotokea katika nchi hiyo.

Maandamano yalizuka nchini Belarus kupinga ushindi wa Rais Alexander Lukashenko katika uchaguzi uliofanyika siku ya Jumapili.

Maelfu ya watu wamekamatwa tangu kuanza kwa maandamano hayo.

Mataifa 27 ya Umoja wa Ulaya yameshutumu uchaguzi huo kwa kusema haukuwa huru na wa haki.

Taarifa ya pamoja ilieleza hakuna usahihi wa hesabu katika matokeo ya uchaguzi.

**DW.**

# HADITHI


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# Mauaji Harusini- 25

Mtunzi anapatikana (0716 350534)

**Na Adam Fungamwango**




"Ni hivi Diana, mimi nilipokuona tu siku ile nilikupenda sana, lakini nilikuwa na yule msichana mwingine, kwa hiyo sikuwa na uwezo wa kukwambia kuwa nakupenda. Kwanza ningeanzaje pale? Halafu ungekataa kwa sababu kulikuwa na mwanamke mwingine. Na kwa sababu nilikuwa nahitaji chakula kwa ajili ya mbwa wangu, niliagiza sahani tatu pale, halafu nikakwambia wewe ukichukue, ukitunze na ukiletee hapa," alisema maneno ambayo taratibu yalianza kumuingia Diana.

"Nia yangu namba moja ulikuwa ni wewe na umekuja, huo mzigo nao ni chakula cha mbwa wangu, kwa sababu ningekwambia uje mwenyewe tu, sidhani kama ungekubali."

"Mhh haya baba umeshinda." Diana alikubali, huku nyuma ya pazia kukiwa na siri kubwa.

Eddy aliamua kumridhisha Diana kwa sababu moja tu. Kutomfanya awe na wasiwasi na asijiulize maswali mengi kiasi cha kuongea kwa watu bila kujua, hasa wahudumu wenzake, kwa sababu yangemfikia Fikiri aliyeangusha kifuko hicho cha sumu.

************************************

"Nachohitaji ni kuangalia hiki chakula kama nina aina yoyote ile ya sumu. Na kama ni sumu basi ni ya aina gani. Basi ni hilo tu." Eddy alimtazama Mkemia Mkuu wa Serikali aliyekuwa ametuna kwenye ofisi yake.

Ilikuwa ni baada ya maongezi ya dakika kumi hivi, Eddy alipotoa kitambulisho na kujitambulisha kuwa ni Afisa Usalama wa Taifa.

Denis Mataruma aliyekuwa ameshika nyadhifa hiyo miezi sita iliyopita, aliinua simu na kumwita mmoja wa wafanyakazi wake.

Alipofika alimtaka kuchukua mkoba aliokuja nao Eddy.

"Humo kuna chakula. Chakula chenyewe ni biriani ya kuku. Kinachotakiwa ni kukipeleka maabara na kutambua kama kuna chembechembe yoyote ile ya kitu kinachohisiwa kuwa ni sumu. Na kama itagundulika kuwa sumu, kinachotakiwa ni kujua ni sumu ya aina gani. Kama hakuna vile vile jibu linatakiwa." Bosi aliamuru na Eddy alipokewa mzigo huo.

"Vizuri Eddy, nadhani baada ya siku mbili kila kitu kitajulikana na ningependa uje wewe mwenyewe hapa hapa uchukue majibu."

"Na ndivyo itakavyokuwa." Alijibu.

************************************

Alijisikia vibaya. Kitendo cha kumsaliti Shani na kutembea na Diana, kilimfanya ajione mkosaji.

Hata hivyo, kuna sauti nyingine kichwani ilimjia ikimwambia kuwa "Umefanya hivyo kwa ajili ya kumsaidia mtu huyo huyo unayempenda."

Ni kweli, asingefanya vile Diana asingemwelewa. Kitendo cha kuchukua chakula hotelini kwa siri, akakihifadhi nyumbani kwake, siku ya pili akakipeleka, halafu asipate sababu yenye mashiko, asingeeleweka.

Sababu ile aliyoitoa kuwa alimpenda Diana ila aliogopa kumwambia kwa sababu alikuwa na Shani, ilisababisha dada huyo kumuamini, vinginevyo angekuwa anajiuliza maswali mengi ambayo yasingekuwa na majibu.

Na kwa tabia ya wanawake angeanza kuwaambia wengine ili kutoa dukuduku moyoni, hivyo alilazimika kufanya naye mapenzi kwa ajili ya kumuaminisha alichokuwa anasema.

Hii yote ni kwa ajili ya kumlinda Shani, mwanamke aliyetokea kumpenda mno. Alijutia nafsi yake, lakini pia hakuna na jinsi kwa sababu aliapa kwake kuwa atamlinda. Alikuwa ametoka kidogo kazini kwenda kula chakula cha mchana. Akiwa amesimamisha gari kabla ya kutoka nje, aliamua kumpigia simu.

"Nijaalie hali yako bibie, umeshinda salama?" "Salama sijui kwako my love." Sauti tamu kutoka upande wa pili.

"Mimi sijambo, hofu kwako sherry, niambie mama?

Eddy alisikia kicheko cha ghafla kutoka kwa Shani ambacho hakujua ni cha nini. Kabla hata hajasema lolote, aliulizwa.

"Hebu rudia tena, umeniitaje?"

"Sherry. Hilo ndilo lililokufurahisha?"

"Ndiyo, unajua neno hilo huwa nalisikia kwenye nyimbo za Kikongo, lakini hata baadhi ya bendi za muziki wa dansi za kiswahili." Alijibu Shani.

"Unajua lina maana gani?"

"Najua, maana yake nilipouliza wanasema ni mpenzi, ila ni aghalabu sana sisi Wabongo kuitana sherry, ndiyo maana nimefurahi."

"Basi inawezekana wewe ukawa mwanamke Mbongo wa kwanza kuitwa sherry." Eddy alitania Shani.

"Vipi umekula?" Shani aliuliza.

Lilikuwa ni swali dogo na lililoolekana halina maana, lakini lilimshtua Eddy.

Mara ya mwisho kuulizwa amekula ilikuwa ni zaidi ya miaka 20 iliyopita, alipoliwa mdogo.

Mama yake mzazi Juliet, ndiye alikuwa anamuuliza kama amekula au la, njaa inamuuma au la, lakini tangu alipokuwa mtu mzima na hadi mama yake alipofariki hakuna binadamu yoyote aliyewahi kumuuliza swali hilo. Lilimpekeka mbali sana.

Taratibu aliendelea kugundua kuwa Shani alikuwa mtu sahihi kwake.

Kwa dunia ya sasa ni aghalabu kukutana na mwanamke ambaye anakujali kiasi kile. Mwanamke ambaye anakuuliza kama umekula au la.

Mwanamke ambaye anajali kila kitu chako, badala ya kujijali mwenyewe.

Tuko kwenye dunia ambayo baadhi ya wanawake wanapokuwa na wapenzi wao wanachojali ni kutimiziwa matakwa yao na hawawajali wenzao.

Bendi ya Bima Lee iliwahi kuimba wimbo mmoja ambayo baadhi ya maneno yake ni kwamba 'thamani ya mapenzi ni kwa yule apendwaye, fadhila ya wanaopenda ni mateso.'

Hayo ndiyo mapenzi ya sasa yalivyo. Lakini kwa Shani siyo. Anaonekana ni msichana anayemjali.

"Bado." Alijibu.

"Kwa nini?"

"Ndiyo nakwenda kula hivi sasa, wewe vipi umekula?" Aliuliza.

"Mimi njaa ilikuwa inaniuma hadi nimepaki gari yangu hapa sehemu, nimeagiza chips, lakini kaniwekea pilipili nyingi." Shani alisema na kumfanya Eddy kuangua kicheko.

"Piga kelele kwa muuzaji 'akeee.'" Eddy alichombeza akinukuu misemo ya kisasa ya akinadada ambayo hayampa tabu Shani kujibu

"Weweee oyoo oyoo oyoooo"

Utani baina ya wapenzi wao wapya wawili uliendelea kwa muda, kabla Eddy hajaamua kuukatisha.

"Basi mpenzi, ngoja nishuke kwenye gari nikale kwanza, wewe mwenzangu hapo unakula ujue."

"Haya sherry."

Eddy aliendelea kuangua kicheko, baada ya Shani naye kumwita sherry.

"Kumbe na wewe ushalipenda hilo neno." "Nimelipenda sana sherry." Eddy alikauka kwa kucheka, halafu akamwambia.

"Nakupenda sana Shani."

"Ahsante sherry, nafurahi kusikia hivyo. Unajua wewe umekuwa sehemu kubwa sana ya furaha yangu hivi sasa."

"Hata wewe pia umenifanya niwe na furaha zaidi, nyumbani na hata kwenye mishemishe zangu.

Ni hivi Shani, nakupenda sana kuliko neno lenyewe. Na nitaendelea kukupenda siku zote. Sikutokukwaza na sipendi kukuona huna furaha. Nitahakikisha nakulinda, uwe na afya, furaha na amani kwa sababu wewe ndiyo faraja yangu. Eddy alisema huku akiteremka kwenye gari na simu yake sikioni.

"Hata mimi nahitaji kukukumbatia, kukubusu, na kukupa maneno matamu, ulale kwenye miguu yangu, nikudekeze, unidekeze, nipate joto lako. Ahsante sana love, nenda kale sasa." Ilikuwa sauti tamu ya Shani ilisikika masikioni mwa Eddy.

Maneno matamu, kutoka kwa msichana mdogo mbichi ambaye kwa sasa alimuona ameanza kuchamka na kujiamini kuliko ilivyokuwa mwanzo, yalimfanya Eddy kufikiria kuongeza nguvu ya kuendelea kuwa naye kama mpenzi, kumfahamu zaidi.

**Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu.**

Kichwani alijua pamoja na ambo ya mapenzi, lakini msichana huyo alikuwa na mambo mengi kichwani yanayomtatiza kama alivyomwambia mwenyewe.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu." alilia Shani.

"Najua. Najua Shani. Tutakuwa wote. Sitokuacha peke yako. Ila kuna siku ningependa uniambie matatizo yote yaliyokupata huko nyuma, yaliyokuwepo na ambayo unaona kama yatakuwa kikwazo kwako." "Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu.

Alikumbuka naneno hayo aliyoambiwa walipokuwa ABC Hotel.

Ndipo Eddy alipokumbuka kuwa jioni ya siku hiyo ilikuwa ni siku ya kwenda kwa Mkemia Mkuu wa Serikali kuchukua majibu ya vipimo vya chakula aliachokichukua ABC Hotel, ambacho yeye alikuwa akikitilia shaka kutokana na kwamba mletaji wa msosi huo alikuwa aliletewa Shani, aliangusha kifuko cha sumu.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



**LETICIA JOHN MUSESE** amepotelewa na Cheti cha elimu ya chuo alichosomea katika chuo cha SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE, Alichomaliza mwaka 2019. Na chenye namba ya mtihan: **MES/E/2015/0007.**
Kwa yeyote atakae kiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/572013/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA, KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 95/2020**

**PASCHAL HASENTH....................................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**PRISCILLA PAULO IFUNYA.............MRUFANIWA**

**KWA PRISCILLA PAULO IFUNYA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na.95/2020 imepangwa kutajwa tarehe 16.09.2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi, mahali - Bukoba Mjini.
Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 10.08.2020.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA**

115856702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA BUKOBA,KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA.159 YA 2020**

**(JALADA ASILIA NO.182/2013)**

**RWEHUMBIZA BUBERWA**
**ERICK BUBERWA ..................................................WADAI**

**DHIDI YA**

**HENRY KAMBUGA..............................................MDAIWA**

**KWA: HENRY KAMBUGA**
**(POPOTE PALE ULIPO)**

Unaarifiwa kuwa kesi Na.159/2020 imepangwa kutajwa tarehe 09/09/2020 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R.Mtei saa 2:00 asubuhi, mahali – Bukoba Mjini.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe/mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja na hukumu kutolewa dhidi yako.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hili leo tarehe 12.09.2020.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA BUKOBA**

115856702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA**

**KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 49 YA 2020**

Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya

**RODNEY MUTIE MENGI...................................... MAREHEMU**

**DHIDI YA**

**REGINA MENGI NA**

**ABDIEL MENGI..........................................................WAOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**

[Kanuni ya 75]

Watu wote wanaodai kuwa na Haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa waombaji hapo.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe **12 Mwezi wa 10 Mwaka 2020**

Hati hii imetolewa **07 Mwezi 08 Mwaka 2020**

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**


*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*






**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# BESIKTAS YAMKANA KWEUPE BALOTELLI




**ROME,** Italia

MARIO Balotelli anaonekana kuwa hana matumaini ya kuhamia Besiktas baada ya Rais wa klabu hiyo, Ahmet Nur Cebi, kusema kwamba straika huyo wa Italia hatakiwi na kocha, Sergen Yalcin.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya Uturuki waliripotiwa kumpa ofa Balotelli, na nyota huyo alionekana kuelekea katika klabu hiyo baada ya kuwa na msimu mbaya kule Brescia.

Rais wa Brescia, Massimo Cellino alibainisha Mei, mwaka huu kwamba anatarajia Balotelli ataondoka katika klabu hiyo ya nyumbani kwake baada ya msimu kumalizika.

Kauli ya Cellino ilikuja baada ya nyota huyo wa zamani wa timu ya Taifa ya Italia mwenye umri wa miaka 30, kushindwa kutokea kwenye mazoezi ya klabu hiyo, madai ambayo yalikanushwa na Balotelli kabla ya Brescia kushuka daraja.

Cebi alibainisha kwamba jina la Balotelli linaweza kuwa kwenye usajili wa timu hiyo, lakini Yalcin hana mpango wa kumchukua mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City pale Istanbul.

Cebi, amenukuliwa na vyombo vya habari vya Uturuki akisema: "Sergen Yalcin hamfikirii Mario Balotelli kama mmoja wa washambuliaji anaowataka. Ameniambia hivyo.

"Watendaji walianza mazungumzo ya awali na mchezaji na kumsikiliza, lakini hilo halina maana kwamba uhamisho wake unaweza kutokea."

# Jimenez aambiwa andoke Wolves

**LONDON,** England

RAUL Jimenez ameambiwa kuwa lazima aondoke ndani ya klabu ya Wolves msimu huu kwenye dirisha la usajili ili akapate changamoto mpya sehemu nyingine.

Nyota huyo amekuwa akihusishwa kuibukia ndani ya Klabu ya Liverpool na Manchester United ambazo zimeonyesha kuwa zinahitaji saini yake jambo lililomfanya mchambuzi wa michezo Kituo cha ESPN ambaye ni raia wa Mexico, Sergio Dipp, kumwambia kwamba ni muda wake wa kupata changamoto mpya.

Jimenez amekuwa bora ndani ya Wolves akitupia jumla ya mabao 17 ndani ya Ligi Kuu England na 10 ndani ya Europa League huku akitoa jumla ya pasi 10 za mabao kwenye mashindano yote.

Raia huyo wa Mexico mwenye umri wa miaka 29, ana nafasi ya kufanya makubwa msimu ujao kutokana na uwezo wake licha ya timu yake kutolewa na Sevilla baada ya kufungwa bao 1-0 kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ni muda wake sasa kuondoka ndani ya Wolves na kwenda kupata changamoto mpya kwenye timu kubwa, uwezo anao, ikiwa ataondoka kwa sasa kutampa mabadiliko makubwa yeye mwenyewe mbeleni."






# Coutinho anataka kurudi kukipiga EPL

**MUNICH,** Ujerumani

PHILIPPE Coutinho anataka kurudi kwenye Ligi Kuu ya England baada ya mkataba wake wa mkopo kumalizika Bayern Munich, lakini bado anaweza kubakia na klabu yake ya Barcelona, kwa mujibu wa wakala wake, Kia Joorabchian.

Coutinho aliondoka England kwenda Barca mwaka 2018 akiwa ametumia miaka mitano na Liverpool, huku klabu hiyo ya Catalunya ikimchukua baada ya kumpoteza Neymar aliyekwenda Paris Saint-Germain.

Uhamisho huo haukuwa na mafanikio sana kwake, kwani msimu wake wa kwanza pale Camp Nou ulikuwa mbaya, ambapo alijikuta akishutumiwa na kuzomewa mara kadhaa na mashabiki wa Barca.

Aliondoka na kwenda Bayern kwa mkopo mwaka jana, huku miamba hao wa Ujerumani wakiwa na kipengele cha kumnunua kwa euro milioni 120.

Lakini alicheza mechi 15 za Bundesliga mwanzoni mwa msimu wa 2019-20, na ilikuja kama mshangao wakati Ofisa Mtendaji wa Klabu hiyo, Karl-Heinz Rummenigge alipothibitisha Mei, mwaka huu kwamba kipengele chake cha manunuzi kimemalizika muda wake.

Coutinho haonekani kama anaweza kuwa na majaliwa ya baadaye kule Barca, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zikionyesha nia ya kutaka kumsajili, ingawa Joorabchian amesema hakuna uamuzi uliofikiwa hadi sasa.

"Kwa wakati huu, Coutinho anafikiria zaidi hatua inayofuata ya Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema wakala wake akiiambia TalkSPORT.

"Hajapata mechi nyingi za kucheza klabu ambayo inammiliki, inaweza kuwa sehemu ambayo atacheza.

"Na nafikiri baada ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kumalizika, na kile kitakachotokea, tutakaa chini na kuzungumza.

"Sijazungumza naye bado kuhusu hilo. Lakini nafikiri Barcelona ndio itakuwa sehemu yake ya kucheza."

# Willian asaini rasmi miaka mi3 Arsenal

**LONDON,** England

Arsenal imethibitisha rasmi kumsajili kwa uhamisho huru winga wa zamani wa Chelsea, Mbrazil Willian ambapo sasa atakuwa akivuta pauni 220,000 kwa wiki akiwa dimba la Emirates.

Kutua kwa Willian (32), kulithibitishwa kupitia akaunti ya mtandao wa kijamii ya Twitter ya 'Gunners' jana asubuhi kwamba amesaini mkataba wa miaka mitatu na kukabidhiwa jezi namba 12.

Na sasa Willian anaelekeza akili yake katika kuibebesha mataji ya Ligi Kuu England na Ulaya akiwa na uzi wa Arsenal baada ya kueleza Mikel Arteta amemshawishi kujiunga na klabu hiyo.

Willian alikuwa mchezaji huru Jumapili baada ya mkataba wake kumalizika pale Chelsea huku pande hizo mbili zikishindwa kufikia muafaka.

Chelsea waliripotiwa kutaka kumpa ofa ya mkataba wa miaka miwili, lakini imedaiwa kwamba Willian mwenyewe alikuwa akitaka mkataba wa miaka mitatu.

Mchezaji huyo hajaficha nia yake ya kutaka kubaki jijini London hata kama hatakuwa Chelsea, na Arsenal ilikuwa ikihusihwa kuwania kumsajili yake kabla ya kufanikisha jana, Ijumaa.





# FERNANDES ATOA SABABU UTD KUTWAA NDOO EUROPA

**MUNICH,** Ujerumani

BRUNO Fernandes anaamini kushinda taji la Ligi ya Europa kutaisaidia Manchester United kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutoa changamoto kwenye Ligi Kuu ya England msimu ujao.

Fernandes alifunga bao la penalti katika muda wa ziada kuisaidia United kupata ushindi wa 1-0 dhidi ya Copenhagen mapema wiki hii na kufuzu nusu fainali ya Ligi ya Europa na sasa watawakabili Sevilla Jumapili.

Kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer kilitolewa kwenye nusu fainali ya Kombe la EFL na FA msimu huu, lakini Fernandes aliyesajiliwa Januari anaamini timu hiyo inaweza kuwa na mafanikio makubwa baada ya kumaliza nafasi ya tatu kweye EPL.

"Nafikiri ni muhimu sana kushinda kwa sababu kila mchezaji anahitaji kuelewa namna gani kushinda taji na Manchester United kulivyo muhimu," alisema Fernandes akinukuliwa na vyombo vya habari vya England.

"Kwa kocha, itakuwa muhimu na kwa wachezaji pia, kwa sababu tumefanya kila kitu kuhakikisha tunafika hatua hiyo.

"Nafikiri tutamaliza na taji, kwani utakuwa mwaka mzuri kwetu na tutapata hamasa nzuri zaidi kwenye Ligi Kuu ya England."

# 'Hongera Leipzig kuitoa Atletico'

**LISBON,** Ureno

DIEGO Simeone hana lawama kwa kikosi chake cha Atletico Madrid baada ya kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, akisisitiza timu yake ilifanya kila kitu lakini RB Leipzig walistahili ushindi.

Leipzig iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Atletico jijini Lisbon Alhamisi wakati Tyler Adams alipofunga la ushindi.

Joao Felix awali alisawazisha bao la ufunguzi la Dani Olmo, lakini Atletico walikuwa kwenye wakati mgumu kuweza kupenya ngome ya miamba hao wa Bundesliga.

Simeone haraka aliwapa hongera Leipzig baada ya kufuzu nusu fainali na sasa watakutana na Paris Saint-Germain.

"Tulifanya kila kitu," alisema akiiambia Movistar. "Ilikuwa ni ngumu kwetu kushinda kwa sababu walikuwa na kikosi chenye kasi sana. "Umekuwa ni mwaka mrefu. Kulikuwa na presha kubwa ya kuja kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Tulikuwa na wiki moja tu ya mazoezi.

"Tulishindwa kucheza kwa namna tulivyotakiwa. Nimeipenda Leipzig. Walikuwa na mwamko mzuri na kiwango cha kuvutia sana na hilo lilitugharimu sisi. Hatuna cha kujitetea."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PERSIE AIPA ARSENAL SIRI AUBAMEYANG KUBAKI

●●● Yeye ni mchezaji wa daraja la juu, na anataka azungukwe na wachezaji wa daraja...

**LONDON,** England

ARSENAL lazima wamuahidi Pierre-Emerick Aubameyang kwamba watasajili wachezaji wa daraja la juu kama wanataka kumshawishi abaki, amesema Robin van Persie.

Mshambuliaji Aubameyang yupo kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake pale kwenye dimba la Emirates na hakuwa tayari kuzungumzia kuhusu majaliwa yake baada ya kushinda Kombe la FA dhidi ya Chelsea, Agosti 2.

Nahodha huyo amekuwa akihusishwa na mpango wa kutaka kuondoka, lakini imeripotiwa kwamba yupo tayari kubakia kwa mimba hao wa London Kaskazini baada ya Mikel Arteta kuteuliwa kuwa kocha mkuu.

**Hakuna makubaliano yoyote yaliyofikiwa na straika wa zamani wa Arsenal, Van Persie amesema klabu lazima imshawishi Aubameyang kwamba wataki jenga kikosi chenye uwezo wa kutoa changamoto kwenye Ligi Kuu na Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Van Persie ameiambia Stats Perform News: "Arsenal wangependa yeye abakie, bado hajaja na uamuzi wake. Aliulizwa swali baada ya kushinda FA na hakuweza kujibu, hivyo sijui.

"Sijui nini anachofikiria, sijui Arsenal wamempa ofa gani na sizungumzii kuhusu fedha, nazungumzia kuhusu wachezaji kwa sababu wachezaji wanamtaka yeye kucheza na wale wa daraja la juu.

"Yeye ni mchezaji wa daraja la juu, na anataka azungukwe na wachezaji wa daraja la juu kabisa."

## ZISIKUPITE

### LIVER HAIPOI KWA ALCANTARA

LIVERPOOL wamewasiliana na miamba wa Ujerumani, Bayern Munich kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29. ***(Bild)***

### PARTEY LULU ARSENAL, JUVE

ARSENAL wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Juventus katika mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Ghana na Atletico Madrid, Thomas Partey, 27. ***(Gazzetta Dello Sport, via Mail)***

### SANCHO HAONDOKI DORTMUND

MKUU wa soka wa Borussia Dortmund, Sebastian Kehl, amethibitisha kuwa mshambuliaji wa England, Jadon Sancho (20), atasalia katika klabu hiyo licha ya kwamba ananyatiwa na Manchester United. ***(MEN)***

### UTD YAJITOSA KWA CHILWELL

MANCHESTER United wapo kwenye mbio moja na Chelsea katika kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili beki wa kushoto wa Leicester City na England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

### OBLAK KUAMUA ATLETICO

GOLIKIPA wa Atletico Madrid na Slovenia, Jan Oblak, mwenye umri wa miaka 27, anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusiana na hatima yake katika klabu hiyo, huku Chelsea wakiwa wanamtaka. ***(AS)***

### ARSENAL, WILLIAN WAMALIZANA

KLABU ya Arsenal itatangaza usajili wa kiungo wa kimataifa wa Brazil, Willian, 32, kwa mkataba wa miaka mitatu wikendi hii baada ya mkataba wa mshambulaji huyo kumalizika pale Chelsea. ***(Telegraph)***

### MAGNO AKATALIWA LIVER

KLABU ya Liverpool haina mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Vasco da Gama, Talles Magno, licha ya tetesi zinazomhusisha kiungo huyo wa miaka 18- kuhamia Anfield. ***(Standard)***

### SMALLING SOKONI UNITED

MANCHESTER United inataka pauni milioni 20 kutoka kwa Roma ambayo inataka kumsajili beki wake, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, ambaye yuko tayari kupunguziwa mshahara ili kujiunga na klabu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu ya Italia. ***(Sun)***

### PIRLO AMKATAA HIGUAIN

KOCHA mpya wa Juventus, Andrea Pirlo, amemfahamisha mshambuliaji wa Argentina Gonzalo Higuain,32, na kiungo wa kati wa Ujerumani, Sami Khedira mwenye umri wa miaka 33, kwamba wapo huru kuondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto. ***(Goal)***

### DYBALA NJIA NYEUPE EPL

MANCHESTER United na Tottenham Hotspur huenda wakapewa nafasi nyingine ya kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Paulo Dybala, 26, kutoka Juventus msimu huu wa majira ya joto. ***(Mirror)***

### SACHO ANOGEWA DORTMUND

JADON Sancho anayelengwa na Manchester United "anafurahia sana" kucheza na kuelekeza timu ya kikosi "maalum"cha Borussia Dortmund. ***(Bild)***

HABARI MICHEZO

## Azam FC yaja na Azam Festival

**Na Saada Akida**

MAANDALIZI ya Ligi Kuu Bara yamezidi kupamba moto na wakati huu, uongozi wa Azam FC umeweka wazi kuwa Agosti 23, mwaka huu watatambulisha jezi mpya pamoja na wachezaji wote watakaocheza msimu wa 2020/21 wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Makao Makuu ya Azam FC, Ofisa Habari wa timu hiyo, Thabiti Zakaria 'Zaka Zakazi', alisema utambulisho huo wa wachezaji wapya waliosajiliwa pamoja na wale waliobaki ndani ya kikosi cha timu hiyo utafanyika katika kilele cha Tamasha lao la Wiki ya Chamazi (Azam Festival).

Alisema katika kilele cha tamasha hilo watakuwa na mechi ya kirafiki ya kimataifa ambayo kwa sasa wapo katika mchakato kuzungumza na timu kutoka nje ya Tanzania.

"Agosti 23 tutatambulisha wachezaji wetu na jezi za msimu mpya kwa kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa, timu bado tupo katika mchakato na mazungumzo na baadhi ya timu kutoka nje, siku hiyo tutakamilisha utaratibu wetu wa usajili," alisema Zakazi huku akiongeza kuwa uzinduzi rasmi wa tamasha hilo ni Jumapili ya wiki hii kwa kuandaa timu za mpira wa miguu pamoja na klabu ya Jogging baada ya kufanya mazungumzo na serikali ya mitaa ya Chamazi na Mbande.

## Yanga Princess yaingia sokoni

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema amesema atafanya usajili makini wa kuboresha kikosi chake ili kuhakikisha msimu ujao wanakuwa vizuri na kuingia katika ushindani mkubwa wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Edna alisema ameona upungufu ya kikosi chake msimu huu na sasa anahitaji kukiboresha kwa kukifanyia kazi katika dirisha hili kubwa la usajili.



Alisema kuna nafasi nyingi ambazo anatakiwa kuboresha ikiwamo ya washambuliaji kwa kutafuta straika anayeona goli ili kuwasaidia kwa msimu ujao.

"Upungufu wetu umesababisha msimu huu kutofikia malengo, hatutaki makosa hayo yajirudie tunatumia vizuri dirisha kubwa la usajili kuleta watu watakaosaidia timu yetu kwa msimu ujao," alisema

Yanga Princess imemaliza msimu wa 2019/20 ikiwa nafasi ya tano kwenye ligi hiyo iliyoshirikisha timu 12 huku Simba Queens ikitwaa ubingwa wakati JKT Queens ikishika nafasi ya pili na Alliance Girls ikimaliza ya tatu.

# YANGA KUZINDULIA WIKI YAO DODOMA

**Na Faustine Feliciane**

UONGOZI wa klabu ya Yanga umesema watazindua Wiki ya Wananchi (Yanga) Agosti 22, mwaka huu jijini Dodoma badala ya Agosti 15, kama ilivyotangazwa awali.

**Awali Yanga walipanga kuzindua wiki hiyo Agosti 15 jijini Dar es Salaam, lakini sasa wameamua kusogeza mbele kwa wiki moja kutokana na mambo mbalimbali kuingiliana.**

Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, Fredrick Mwakalebela, jana aliweka wazi kuwa baada ya uzinduzi huo jijini Dodoma ratiba zitaendelea kama zilivyopangwa na kilele chake kitafanyika Dar es Salaam.

Alisema katika wiki hiyo masuala mbalimbali ya kijamii yatafanyika yakiwahusisha mashabiki, wanachama, viongozi na wachezaji wa klabu hiyo.

"Tutazindua Wiki ya Wananchi jijini Dodoma, awali ilikuwa tufanye Agosti 15, lakini sasa tumepanga Agosti 22, hivyo ratiba nyingine mpaka kufika siku ya kilele itaendelea kutolewa," alisema Mwakalebela.

Yanga pamoja na mambo mengine wanatarajia kutumia wiki hiyo kuwatangaza mbele ya mashabiki wachezaji wake wapya waliowasajili kwa ajili ya msimu mpya wa Ligi Kuu utakaoanza mapema mwezi ujao.

Awali Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, Hassan Bumbuli alipinga hatua ya kusogeza mbele kwa wiki yao kuwa ni kwa ajili ya kupisha 'Simba Day' ambayo imeanza rasmi jana.

Bumbuli alisema wamepeleka mbele uzinduzi wao kutokana na muingiliano wa ratiba.

"Hatuiogopi timu yoyote, hao Simba na wiki yao wanawalenga mashabiki wao kama ilivyo kwetu pia Wiki ya Wananchi inawalenga mashabiki wa Yanga kwa hiyo hatuwezi kuwaogopa, ni kwa sababu tu mambo yameingiliana na tunataka kulifanya jambo hili kwa ukubwa wake kwa sababu Yanga ni timu kubwa," alisema Bumbuli.

SASA RASMI...




Mshambuliaji mpya wa Simba, Charles Ilanfya, aliyejiunga na klabu hiyo akitokea KMC FC, akiwa amevaa uzi mpya utakaotumiwa na miamba hiyo msimu wa 2020/21 wakati akitambulishwa rasmi jana. **PICHA: SIMBA**

## *Mkwasa amrithi Mayanga Ruvu Shooting*

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Ruvu Shooting umeingia mkataba wa miaka miwili na aliyekuwa Kocha Msaidizi wa Yanga, Boniface Mkwasa kukinoa kikosi cha Ruvu Shooting kwa msimu wa 2020/21, Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema wameingia mkataba na Mkwasa kuchukua nafasi ya Salum Mayanga aliyekuwa kocha wa timu hiyo aliyemaliza mkataba wake.

Alisema baada ya Mayanga na uongozi huo kukubaliana kwa kutomuongezea mkataba, wamemchukuwa Mkwasa kwenda kuendeleza pale alipoishia kocha mwenzake.

"Mkwasa hapa ni nyumbani, hivyo amerejea kuleta mabadiliko ataendelea pale alipoishia mwanafunzi wake Mayanga, tuna imani na kocha huyo wa sasa kufanya makubwa na timu yetu kucheza soka la Barcelona," alisema Bwire.

Alisema baada ya kusaini mkataba na kocha huyo amependekeza baadhi ya wachezaji wa kusajiliwa na tayari wako katika mchakato na utaratibu wa kuweza kupata huduma za nyota hao ambao wengine wanaweza kupatikana kwa mkopo.

"Kwa sasa hatuwezi kutaja majina ya wachezaji hao kwa sababu bado tupo katika mazungumzo na viongozi wao, kwani bado wana mikataba, wanaweza kutolewa kwa mkopo, lakini kwa wale waliokuwa huru tunaogopa bado hatujamalizana nao," alisema Bwire.

Taarifa za ndani zilizolifikia gazeti hili zinaeleza nyota hao ni Iddi Kipagwile, Bryson Raphael kutoka Azam FC, lakini tayari Kipagwile ametua Namungo FC.

# Michezo

Jumamosi Agosti 15, 2020

Nipashe




Persie aipa Arsenal siri Aubameyang kubaki UKURASA 22

BEKI KISIKI...



Beki kisiki Mkenya Joash Onyango, akitia dole gumba katika mkataba wake wa kujiunga na Simba jana, mbele ya Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola. Joash amejiunga na timu hiyo akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya. **PICHA: SIMBA**

## Simba yatangaza beki kisiki, straika

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wameanza kuweka hadharani vifaa vyao vipya kuelekea msimu ujao kwa kumtambulisha beki kisiki Mkenya Joash Onyango aliyejiunga na klabu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili akiwa mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba na Gor Mahia ya Kenya.

Mbali na beki huyo pia jana ilimtambulisha rasmi mshambuliaji Charles Ilanfya aliyejiunga na klabu hiyo akitokea KMC FC, sambamba na jezi zao mpya.

Ilanfya amekamilisha usajili wa kujiunga na Simba baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu kutokana na kuwa katika kiwango bora msimu uliomalizika akiwa mhimili kwenye safu ya ushambuliaji ya KMC.

Katika taarifa ya Simba jana ilieleza: "Nyota huyo mrefu mwenye mwili mkubwa amekuja kuongeza nguvu katika idara ya ushambuliaji akisaidiana na nahodha John Bocco na Medie Kagere, hivyo usajili wake unatarajiwa kuwa mzuri na wenye mafanikio kutokana na uwezo wake pamoja na kujituma."

Ilanfya ambaye pia amewahi kuichezea Mwadui FC, msimu uliomalizika amemaliza na mabao sita.

# YANGA YAIBUA MAZITO HUKUMU YA MORRISON

## ●●● Yasema kwa haya haiwezekani, yamwaga 'upupu', TFF yawapa hukumu sasa mguu na njia CAS...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kumpa ushindi kiungo Mghana Bernard Morrison dhidi ya Yanga katika kesi yao iliyosikilizwa kwa siku tatu mfululizo, uongozi wa klabu hiyo umekuja na mazito dhidi ya shirikisho hilo.

**Morrison ambaye amesaini kuitumikia Simba msimu ujao kabla hata ya hukumu ya kesi hiyo, alikuwa akiilalamikia klabu yake hiyo ya zamani kuwa imeghushi saini yake katika mkataba wa miaka miwili inayodai kuingia naye baada ya ule wa awali wa miezi sita kumalizika.**

Lakini kamati hiyo ikiwa chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala baada ya kupitia nyaraka mbalimbali na mkataba huo, ilimpa ushindi Morrison kwa kueleza kwamba kulikuwa na upungufu makubwa upande wa tarehe ambapo kuna sehemu ilionyesha kuwa amesaini Machi 20 huku chini ikionyesha amesaini Julai 15, 2020.

Mwanjala pia alisema kuna ukurasa wa saini kwenye mkataba huo unaonyesha upungufu katika sehemu ya saini ambayo imefutwa kwa kalamu jambo ambalo linaonyesha kwamba kulikuwa kuna tatizo kwenye masuala ya mkataba.

Lakini jana uongozi wa Yanga ulisema hauna imani na Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya TFF, pamoja na kulitaka Shirikisho la Soka nchini kujitathimini katika uundaji wa kamati nyeti kama hiyo huku ikiwa na kiongozi wa klabu ya upande wa pili ('Simba').

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mwenyekiti wa Yanga, Dk. Mshindo Msolla, alisema wameitilia mashaka kamati hiyo kwa kitendo cha kukaa siku tatu kutoa uamuzi huo.

Alisema shauri hilo kusikilizwa siku tatu huku ndani ya kamati hiyo kukiwa na mjumbe wa upande wa pili, uamuzi uliotoka haukuwatendea haki.

"Kitendo cha uamuzi wa kamati hiyo, kimetufedhehesha sisi viongozi kwa kuonekana wababaishaji katika suala hili la shauri la mchezaji Bernard Morrison kwenye mkanganyiko wa mkataba ambao umetolewa uamuzi.

"Mbali na kuonewa katika shauri la Morrison, lakini pia kuna mambo mengi juu ya mchezaji huyo tukipeleka TFF hayafanyiwi kazi ikiwamo ile sauti ya nyota huyo kudai kuna kiongozi wa upande wa pili kumrubuni, hilo halijatolewa ufafanuzi na wakawa kimya," alisema Msolla.

Alisema katika shauri la Morrison pia amesikitishwa na mwanasheria wa TFF (hakutaja jina), kusema kwamba dola 25,000 amerudisha huku akiikana saini ya mwenyekiti huyo.

"Hizi kauli za mwanasheria huyo zimetupa mashaka kwamba alijuaje hizo pesa zimerudishwa, lakini pia saini yangu ameijuaje, hii inaonyesha kwamba anatetea upande wa pili," alisema mwenyekiti huyo.

Alisema kitendo cha Morrison kusaini Simba ilhali kesi bado haijatolewa uamuzi, pia kitendo cha nyota kumshukuru mjumbe katika kamati hiyo baada ya shauri kutoka, kimewapa mashaka dhidi ya kamati hiyo.

Alisema wanachosubiri hukumu ya kamati hiyo ili wafikishe malalamiko yao Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi ya Mambo ya Michezo, CAS.

"Hatuwezi kupeleka "review" (kuomba kupitiwa upya mwenendo wa kesi hiyo) katika kamati hiyo, baada ya kupata hukumu, tunaenda juu kwani ukiangalia kamati ambayo imetoa uamuzi huo ndio watakaokaa tena kujadili," alisema Msola.

Kwa upande wa mwanasheria wa Yanga, Alex Mgongolwa, alisema hoja ilikuwa juu ya nyota huyo kusaini mkataba na kwamba kuhusu upungufu ya kimkataba ilikuwa hoja nyingine.

"Kwa kitendo cha kamati kumtaka mchezaji kurudisha dola 25,000 inaonyesha kwamba amesaini mkataba ndio hoja iliyokuwapo mezani, hivyo Morrison alisaini mkataba wa miaka miwili kwa dau la dola 50,000 na mshahara wa dola 5,000 kwa mwezi," alisema.

Hata hivyo, jana Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ilitoa hukumu hiyo kwa Yanga.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >